

www.ccoq.org

Aprili – Juni 2021

UNABII WA HABARI ZA BIBLIA


**MPANDA
Farasi wa Pili:
Farasi Mwekundu wa Vita**

**Kwa Nini Mungu
Anaruhusu Mateso?
Je! Kuna Kusudi la Mateso?**


**Kwa Nini Mungu
Alikuumba?**

YKwa kweli, **MUNGU** Ana
Mpango na **WEWE** Binafsi

UNABII WA HABARI ZA BIBLIA



8



18



30

KATIKA MAKALA HII:

- 2 **Kutoka kwa Mhariri: Farasi wa Pili wa Ufunuo** Je!Mpanda farasi ameanza kumwendesha?
- 8 **Somo la 19b: Kwa NINI Agano Jipya?** Biblia Inafundisha Nini?
- 18 **Kwa Nini Mungu Anaruhusu Mateso?** Je!Kuna Kusudi la Mateso?
- 21 **Kwa Nini Mungu Alikuumba?** Kwa kweli, Mungu Ana Mpango na WEWE Binafsi.
- 30 **Miujiza ya Yesu, Sehemu ya 2 – Mtu wa Ukoma Ameponywa** Somo fupi kwa watu wachanga na hata wachanga kwa mioyo.
- 31 **Swali na Majibu** Kanisa lina sehemu gani katika kupoza na ndoa ya watu wa mbari tofauti?

Jalada la Nyuma: Mtandao na Redio Hapa panaonyesha mahali ambapo ujumbe katika maandiko na yale ya kutazamwa wa Kanisa la Mungu *Linaloendelea* unapatikana. *Linaloendelea*.

Kuhusu Jalada la Mbele: Mchoro uliobuniwa na Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) unaohusu mwendeshaji wa farasi mwekundu wa Ufunuo 6.

Unabii wa Habari za Biblia inchapishwa na Kanisa la Mungu *Linaloendelea* (CCOG) 1036 W. Grande Ave., Grover Beach, CA 93433 <https://www.ccog.org>

©2021 Kanisa la Mungu Linaloendelea. Imechapishwa Marekani. Haki zote zimehifadhiwa.

Kunakili Makala yote ama sehemu yake pasipo na ruhusa ya kimaandishi toka kwa mmiliki hairuhusiwi. Tunaheshimu haki zako hivyo hatutoi, kuuza ama kukodisha orodha ya mawasiliano yetu. Endapo haungependa kuendelea kupokea gazeti hili, wasiliana na afisi yetu ya Grover Beach. Maandiko

yamenukuriwa toka New King James Version © Thomas Nelson, Inc, Publishers, used by permission isipokuwa pale tu tumeelekezwa vinginevyo.

Unabii wa Habari za Biblia HUWEZESHWA KWA MICHANGO YENU.

Unabii wa Habari za Biblia HUWEZESHWA KWA MICHANGO YENU.

Mhariri Mkuu: Bob Thiel

Makala/Mhariri Msaidizi: Joyce Thiel

Mashahihisho: John Hickey

SBC Course Assister: Shirley Gestro.

Mfasiri: Ondigo Ochieng

Imeundwa na: James Erwin Estoque

Picha: Picha zote zimetokana na familia ya Thiel ama na vyanzo vya mitandao ya kijamii kama vile Wikipedia, picha za milki za umma.



MPANDA FARASI WA PILI: FARASI MWEKUNDU WA VITA.

Yesu alitoa onyo kuhusu vita na matetesi ya vita kama sehemu ya mwanzo wa utungu:

6 Nanyi mtasikia habari za vita na matetesi ya vita; angalieni, msitishwe; maana hayo hayana budi kutukia; lakini ule mwisho bado. 7 Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na njaa, na matetemeko ya nchi mahali mahali. 8 Hayo yote ndiyo mwanzo wa utungu. (Mathayo 24:6-8).

Tazama pia yale ambayo Kitabu cha Ufunuo Sita kinasema kuhusu mpanda farasi wa pili:

3 Na alipoifungua muhuri wa pili, nikamsikia yule mwenye uhai wa pili akisema, Njoo! 4 Akatoka farasi mwingine, mwekundu sana, na yeye aliyempanda ana uta, akapewa taji, naye akatoka, ali akishinda tena apate kushinda. (Ufunuo 6:3-4)

Ukilinganisha pia mpanda farasi wa pili wa Ufunuo 6:3-4, utapata kwamba Yesu alionya kuhusu vita:

Tazama kile ambacho Kanisa la Mungu la awali Ulimwengu kote lilifundisha katika mwaka wa 1973, kwamba kitatukia baada ya mpanda farasi wa kwanza:

Katika ile harakati ya mpanda farasi wa kwanza “kushinda ali alikishinda” kwa kutumia dini ya uongo, mpanda farasi wa pili-yaani vita-atafanya hima kama chombo cha ushindi. (Alexander G, uk. 23-24)

Twapaswa kujua kwamba ijapokuwa kanisa la awali la Mungu ulimwengu kote lilionya kwamba wapanda farasi wote watakuja kwa upesi moja baada ya mwingine, maelezo yafuatayo ya Yesu yanapendekeza

kwamba kuna mwanya kwa wakati wa matukio:

8 Akasema, Angalieni, msije mkadanganyika, kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, Mimi ndiye; tena, Majira yamekaribia. Basi msifuate hao. 9 Nanyi mtakaposikia habari za vita na fitina, msitishwe; maana hayo hayana budi kutukia kwanza, lakini ule mwisho hauji upesi.” (Luka 21:8-9)

Wakati ambapo muda huo utachukua haujatajwa, lakini maandiko hayo yanapendekeza kwamba kutakuwepo na muda. Muda au mwanya ambao twapatikana ndani yake.

Kumbuka kwamba kufungua kwa muhuri wa pili (Ufunuo 6:3-4) kutaleta ukosefu wa amani duniani.

Wakati anaitwa farasi mwekundu wa kawaida (ama mpanda farasi mwekundu) wa vita, lakini haijatajwa vilevile. Kumbuka kwamba “anaondoa amani duniani Ili kwamba watu wauane.” Je! Yawezakuwa matukio ya mwaka 2020, kama vile Homa ya Korona yanaweza kulinganishwa na “kuondoa amani duniani”?

Katika ulimwengu mzima watu WAMEOGOPA. Hisia za hali ya kawaida imepotea kote ulimwenguni. Kumbuka kwamba kizuio cha usafiri ni kwa sababu ya uwoga. Maafisa wa vyombo vya habari na serikali wanasema kwamba hali ya kawaida haitakuwepo tena na kwamba tunapaswa kukubali kile ambacho wanakiita “hali mpya.” Je! Kwa kuvisia, hali hii yawezakuwa kufungua kwa muhuri wa pili?

Tangia vita vya pili vya ulimwengu, hatujawahi kuona tukio lolote ambalo limeathiri dunia nzima kama hili. Ninahisi kwamba pengine muhuri wa pili ulifunguliwa mwisho wa Majira ya Machipuko ya mwaka 2020 ama hata Majira ya Kupukutika ya mwaka 2019. Kwa hivyo pengine twaweza kutazama kufungua kwa muhuri wa pili kama iwezekanavyo.

Neno la kawaida la Kiyunani la “amani” (εἰρήνη) ambalo limefasiriwa kama eirēnēn) katika Ufunuo 6

pia linaweza kufasiriwa kumaanisha kuondoa ustawi pia (tazama BibleHub.com). Homa ya Korona,kwa kiwango fulani,kimefanya hivyo. Watu wameogopa na pia hawana uwazi kwa kiwango kile hatujawahi kuona ulimwenguni kote kwa wakati wowote katika karne ya 21.Maandishi ya Barnes kuhusu Biblia yanasema:

Nguvu aliyopewa yule akaaye kwenye farasi: na alipewa nguvu yule akaaye juu ya farasi ili apate kuondoa amani duniani,na wapate kuuwana . Hii ina maana kwamba hali iliyokuwa kabla ya hali hii ilikuwa ya utulivu,na kwamba hali iliyofuata ilileta ugomvi na kumwaga damu. Dhana hii ilithibitishwa na maneno ya awali - τῆν εἰρήνην tēn eirēnēn - "amani"; yaani,amani iliyokuweco zamani. Wakati amani ya kawaida inarejelewa,neno hili linatumiwa bila nakala inayopatikana kwenye fungu hili: Mathayo 10:34, "Msidhani kuwa nimekuja kuleta amani - βαλεῖν εἰρήνην balein eirēnēn - duniani."

Kwa hivyo,huyu mpanda farasi sio wa vita peke yake,lakini anahusika na kuondoa amani.

Kumbuka kwamba kimaandiko,kuondoa amani au ustawi na mpanda farasi mwekundu haitaziua mkataba wa amani wa Danieli 9:27.

Pia haitaziua Siri ya Babeli Mkuu kwa kuwa na wakati wa kustawi (hakika kulingana na Danieli 11:39-43,vita vitaleta utajiri na ustawi kwa Mfalme wa Kaskazini. Mwendeshaji wa farasi huyu SIO kwamba ataleta vita vya kawaida (japo vita vya kawaida vimenenwa na Yesu katika Mathayo 24,Marko 13,na Luka 21).

Lakini mambo yataenda mrama.

Kanisa la Mungu la awali ulimwenguni kote(WCG) liliandika yafuatayo mnamo 1975:

Mwisho wake utakuwa wapi? Hili ndilo swali wale wanafunzi wa Yesu waliuliza katika Kitabu cha Mathayo ishirini na nne. Jawabu la Yesu,linalojulikana kama Unabii wa Mizeituni,unatoa ufunuo "Nanyi mtasikia habari za vita na matetesi ya vita," Kristo alisema hivyo,akirejelea mmojawapo ya ishara ambayo itatangaza mwisho wa nyakati (mstari wa 6).

Hakika vita vimekuwako kila mara. Na hakika maneno ya Kristo yalikuwa na maana haswa

kwa siku na wakati . Baada ya muda wa miongo michache,kikosi cha Warumi chini ya amri ya Tito,walibomoa na kuchoma mji wa Yerusalemu.

Lakini onyo la Yesu kuhusu vita pia lilikuwa linaangazia kipindi kingine katika historia. Katika Kitabu cha Ufunuo,Kristo akiongea kupitia kwa Mtume Yohana,alieleza baadhi ya maelezo yake ya awali. Katika sura ya sita,Yohana aliandika: "Akatoka farasi mwingine,mwekundu sana,na yeye aliyempanda alipewa kuiondoa amani katika nchi,ili watu wauane,naye akapewa upanga mkubwa" (Ufu. 6:4).

Yohana hakuwa anazungumzia kuanguka kwa mji wa Yerusalemu. Vita hivyo vya Yerusalemu vilikuwa vimekwisha kufanyika miaka ishirini iliyopita akiwepo. Yohana alikuwa alirejelea matukio yatakayofanyika baadaye ambayo yatafanya miaka 6000 ya historia ya binadamu kufikia mwisho wa uharibifu ... **Yohana anarejelea nyakati ambazo zitakuja baadaye wakati ambapo "kuishi kwa amani" kitakuwa kitu kilichopitwa na wakati. ...**

Ndiyo maana Yeremia kwa kueleza kuhusu nyakati hizi za hatari alisema,: "Ole! Maana siku ile ni kuu,hata hapana inayofanana nayo,maana ni wakati wa taabu ya Yakobo ..." (Yer. 30:7). (Ritter G. 4 Horsemen of the Apocalypse - The Red Horse - War, pp. 48, 52; see also Ritter R. The War that could end it all. Good News, December 1975)

Kuna uwezekano wa vita kuweco katika sehemu za ulimwengu ambazo hazijawahi kuwa na vita (pengine,kwa mfano,kati ya mataifa ya Marekani ya Kusini), pia vita katika maeneo ambayo yamekuwa na vurugu (kama vile Korea,haswa vita vinavyohusu maitaifa ya Asia; Azerbaijani na Armenia). Dameski hatimaye itaharibiwa na itakuwa ishara ya uharibifu utakaowajia Yakobo(Isaiah 17:1-4). Kutakuwako na vurugu na pengine ghasia kwa kiwango ambacho hakijaonekana bado, pamoja na miongoni mwa mataifa ya Magharibi(kama vile Uropa na Marekani Kaskazini). Jambo hili litasababisha viongozi wa vita kuchipuka katika sehemu nyingi za ulimwengu. Na Ulaya (Mfalme wa Kaskazini wa mwisho) ,baada ya matangazo ya mikataba mingi ya uongo (k.v. Danieli 9:26-27; 11:27; 1 Wathesalonike 5:3), atakuwa kiongozi

wa mwisho wa Mnyama (Ufunuo 13:4) na atateka nyara mataifa mengi (Danieli 11:39-43).

Ulaya “Mfalme wa Uropa”

Unabii unaofuata usio wa Kibiblia unaonekana kufundisha kwamba “Mfalme wa Uropa” anayekuja atakuwa kama Mnyama wa Ufunuo:

Nostradama (karne ya 16): Wakati Griffini Mfalme wa Uropa atakapokuja, Akiongozwa na Akuila. Watu wekundu na weupe wataongoza jeshi kubwa ... (Dupont, Yves. Unabii wa Katoliki: The Coming Chastisement. TAN Books, Rockford (IL), 1973, p. 105)

Griffini ni kiumbe cha hekaya ambacho kina sehemu nyingine za wanyama kama kichwa cha simba mbawa za tai, na samaki (Dupont, p. 105). Aina moja inajulikana kama “griffini ya bahari” na inafanana na joka katika sura yake, kwa hivyo Griffini yuawezakuwa kama mnyama utokao baharini (Ufunuo 13:1) ambaye pia ana mdomo kama ya simba (cf. Danieli 7:4; Ufunuo 13:2). Katika hekaya, Akuila (kundi la nyota) ilikuwa inamilikiwa na mungu wa Rumi Jupita na alikuwa akimfanyia kazi nyingi (Aquila. Wikipedia, accessed 02/07/11).

Kwa hivyo, Nostradama “Mfalme wa Uropa” yaani Griffini alionekana kufanana na Mnyama wa Biblia. Na hata pia “Mfalme Mkuu” (ambaye anadhaniwa kuwa ni mtu) aliyetabiriwa na baadhi ya Wakatoliki Wakigiriki-Rumi:

Mstahiki Bartholomew Holzhauser (aliyeaga mwaka wa 1658): Mtawala Mkuu atakuwa na msaada wa kipekee wa Mungu na hatashindwa. (Connor E. Prophecy for Today. Imprimatur + A.J. Willinger, Bishop of Monterey-Fresno; Reprint: Tan Books and Publishers, Rockford (IL), 1984, pp. 35-36)

Kwa hivyo, kiongozi mwenye nguvu ya vita anatarajiwa kulingana na unabii wa kibiblia na wa Kirumu au Othodoksi--ijapokuwa Biblia inaonyesha kwamba msaada wa “mtawala” huyu utakuwa wa Kishetani (Ufunuo 16:13), sio msaada wa Mungu. Biblia inatabiri kuhusu Kiongozi wa Uropa anayelitwa “Mnyama” (Ufunuo 13:3-4) na “Mfalme wa Kaskazini” (Danieli 11:40).

Kwa vile kuna uasi dhidi ya Mnyama/Mfalme wa Kaskazini katika Danieli 11:40, ni wazi kwamba ijapokuwa mpanda farasi ameanza rasmi kuendesha farasi kabla ya Dhiki Kuu (na pengine ameanza tayari), atamaliza baada ya Dhiki Kuu kuanzishwa.

Biblia inaonyesha kwamba Kiongozi wa Ulaya/Uropa atachipuka AKINENA juu ya amani, lakini atakuwa kiongozi wa vita na mateso (Ufunuo 13:1-10; Danieli 11:31-44).

25 Na kwa mashauri yake atafanikisha hila mkononi mwake; naye atajitukuza nafsi yake moyoni **mwake; naye atawaangamiza wengi katika hali yao ya salama;** naye atasimama kushindana naye aliye Mkuu wa wakuu; lakini atavunjika, bila kazi ya mikono. (Danieli 8:25).

23 **Na baada ya maagano atatenda kwa hila; maana atapanda, naye atakuwa** hodari pamoja na watu wadogo. 24 **Wakati wa amani atapaingia mahali palipofanikiwa sana pa wilaya hiyo;** nayo atatenda mambo ambayo baba zake hawakuyatenda, wala babu zake; atawafanya kati yao mawindo, na mateka, na mali; naam, atatunga hila zake juu ya ngome, hata wakati ulioamriwa. (Danieli 11:23-24)

Kwa hivyo, kiongozi huyu anaonyesha watu kwamba kutakuwa na “amani” huku akishiriki katika aina fulani ya mkataba. Kiongozi huyu pia anaitwa “mfalme” wakati anathibitisha agano lisilodumu katika Danieli 9:27-huyu ni Kiongozi wa Uropa.

Huzuni na Farasi Mwekundu wa Vita

Lakini kumbuka kwamba Yesu alisema:

4 “Angalieni, mtu asiwadanganye. 5 Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, Mimi ni Kristo; nao watadanganya wengi. 6 **Nanyi mtasikia habari za vita na matetesi ya vita; angalieni, msitishwe;** maana hayo hayana budi kutukia; lakini ule mwisho bado. 7 Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na njaa, na matetemeko ya nchi mahali mahali. 8 **Hayo yote ndiyo mwanzo wa utungu.** (Mathayo 24:4-8)

Kanisa la awali ulimwenguni kote (WCG) lilichapisha yafuatayo:

."Kwa hakika neno "UTUNGU" linamaanisha "majaribu" au "dhiki". "Kwa hivyo Yesu anasema kwamba huo ndio mwanzo wa "dhiki" {ambao utaongoza } — kwenye Dhiki Kuu. (Antion D. Will You Fall Away? Good News. May-June 1968)

Tuko katika "mwanzo wa utungu." Kile ambacho kinafanana na mpanda farasi wa kwanza wa unabii wanaosambaza injili ya uwongo wa muungano wa madhehebu mbalimbali na ekumeni ambayo imezidi kuwa na umaarufu katika ulimwengu miaka mingi iliyopita. Wanadai kwamba Yesu ndiye Kristo,lakini hawaenendi kulingana na madai hayo,na wanadanganya wengi.

Yesu alisema kwamba baada ya udanganyifu kutakuwa na vita na matetesi ya vita.

Maoni ya viongozi wa Marekani,Korea Kaskazini na Irani yanaenda sambamba na maelezo hayo.Pia kuna masuala na Israeli,Siria,Hong Kong,Kokasas,Wapalestino,na sehemu za Afrika na mahali mbalimbali.

Hakijaanza bado,twawezakuwa karibu sana na wakati wa mwisho wa mpanda farasi mwekundu wa unabii.

Duru ya vita inaandama sehemu nyingi ya ulimwengu hivi sasa. Hata kama tunatarajia kuona amani usiodumu katika sehemu nyingi kama Mashariki ya Kati baada ya migogoro (Danieli 9:27), wengi wanajiandaa kwa vita.

Kufunguliwa kwa muhuri wa pili SIYO Dhiki Kuu, kwa sababu Dhiki haiwezi kutokea kabla ya kufunguliwa kwa muhuri wa tano (Ufunuo 6:9).

Yesu alisema kwamba kabla ya Dhiki Kuu (Mathayo 24:21), tunatarajia kuona vita ,matetesi ya vita,na huzuni tofauti tofauti (Mathayo 24:4-8).

Hata hivyo,viongozi wa ulimwengu,pasi na Mnyama wa Ufunuo 13:1-10,wanashirikiana na mnyama mwekundu.

Nini inaongoza uendeshaji wa mpanda farasi,pamoja na yule wa vita?

Shetani!



Mpanda Farasi Mwekundu wa Vita

7 Kulikuwa na vita mbinguni;Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka,yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake;8 nao hawakushinda,wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni.9 Yule joka akatupwa,yule mkubwa,nyoka wa zamani,aitwaye Ibilisi na Shetani,audanganye ulimwengu wote. (Ufunuo 12:7-9)

12 Ole wa nchi na bahari! Kwa maana yule Ibilisi ameshuka kwenu mwenye ghadhabu nyingi,akijua ya kuwa ana wakati mchache tu. (Ufunuo 12:12)

Shetani amedanganya ulimwengu,na hata dini (2 Wakorintho 11:14-15),pia ni chanzo cha uendeshaji wa farasi mweupe ukifuatwa na vitu vingine..

Mnyama wa Vita

Shetani anazua vurugu kote ulimwenguni.Na anazua vita na vurugu kule Ulaya.

Biblia inaonyesha kwamba kiongozi anayependa vita atainuka kule Uropa:

1 Kisha nikaona mnyama akitoka katika bahari,mwenye pembe kumi,na vichwa saba,na juu ya pembe zake ana vilemba kumi,na juu ya vichwa vyake ana majina ya makufuru.2 Na yule mnyama uliyemwona alikuwa mfano wa chui,na miguu yake ilikuwa kama miguu ya dubu,na kichwa chake kama kichwa cha simba,yule joka akampa nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi.3 Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la

mauti,na pigo lake la mauti likapona.Dunia yote ikastaajabia mnyama yule.⁴ Wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa huyo uwezo wake;nao wakamsujudu yule mnyama,wakisema,Ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye? (Ufunuo 13:1-4)

Bahari hiyo,kulingana na Danieli,ni “Bahari Kuu” (Danieli 7:2-8), ambayo pia inatambulika na maandiko mengine kwa jina Bahari ya Mediterania (Hesabu 34:6-7; Joshua 1:4; 9:1; 23:4; Ezekieli 47:13-16).

Wakati huyu mnyama ataamua kufanya vita vikubwa,mwanzoni atafaulu.

Kabla ya hiyo,atasababisha ghasia (ama vita vya umma) katika Ulaya. Kwa vile anahusika katika Danieli 9:27 na kusababisha vita na vurugu,atatambulika kama mleta amani.

Atageuka dhidi ya Marekani na ndugu zake wanaozungumza lugha moja:

24 Na nguvu zake zitakuwa nyingi mno,lakini si kwa uwezo wake mwenyewe;naye ataharibu kiasi cha kustaajabisha watu,na kufanikiwa,na kutenda apendavyo;naye atawaangamiza hao walio hodari na watu watakatifu.²⁵ Na kwa mashauri yake atafanikisha hila mkononi mwake;naye atajitukuza nafsi yake moyoni mwake;naye atawaaangamiza wengi katika hali yao ya salama;naye atasimama kushindana naye aliye Mkuu wa wakuu;lakini atavunjika,bila kazi ya mikono. (Danieli 8:24-25)

39 Naye ataziteka nyara ngome zenye nguvu kwa msaada wa mungu mgeni;na yeye atakayemkubali atamwongoza kwa utukufu;naye atawapa kumiliki wengi;naye atagawa nchi kwa rushwa. (Danieli 11:39)

Huyu kiongozi ambaye pia anaitwa Mfalme wa Kaskazini,atawaangamiza na kuharibu nchi zinazomikiliwa na Waislamu:

40 na wakati wa mwisho mfalme wa kusini atashindana naye;na mfalme wa kaskazini atamshambulia kama upepo wa kisulisuli,pamoja na magari ya vita,na wapanda farasi,na merikebu nyingi;naye ataingia katika nchi hizo,na kufurika na kupita katikati. ⁴¹ Tena ataingia katika hiyo

nchi ya uzuri,na nchi nyingi zitapinduliwa;lakini nchi hizi zitaokolewa na mkono wake,Edomu,na Moabu,na wakuu wa watu wa Amoni.⁴² Naye ataunyosha mkono wake juu ya nchi hizo,hata na nchi ya Misri haitaokoka.⁴³ Lakini atakuwa na nguvu juu ya hazina za dhahabu na fedha,na juu ya vitu vyote vya Misri vyenye dhamani;na Walibia na Wakushi watafuata nyayo zake. (Danieli 11:40-43)

Atafanikiwa kivita kwa muda. (Ufunuo 13:4).

Shetani atahitaji kuona wengi wakiharibiwa na ataongoza mataifa kukusanyika katika Armagedoni:

13 Malaika wa sita akapiga baragumu,nikasikia sauti moja iliyotoka katika zile pembe za madhabahu ya dhahabu iliyo mbele za Mungu,¹⁴ ikimwambia yule malaika wa sita aliyekuwa na baragumu,Wafungue nao malaika wanne waliofungwa kwenye mto mkubwa Frati.¹⁵ Wale malaika wanne wakafunguliwa,waliokuwa wamewekwa tayari kwa ile saa na siku na mwezi na mwaka,ili kwamba waue theluthi ya wanadamu.¹⁶ Na hesabu ya majeshi ya wapanda farasi ilikuwa elfu ishirini mara elfu kumi;nilisikia hesabu yao . (Ufunuo 9:13-16)

13 Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura,zikitoka katika kinywa cha lile joka,na katika kinywa cha yule mnyama,na kutoka katika kinywa cha yule nabii wa uongo.¹⁴ Hizo ndizo roho za mashetani,zifanyazo ishara,zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi. (Ufunuo 16:13-14)

16 Wakawakusanya hata mahali paitwapo kwa Kiebrania Har-Magedoni. (Ufunuo 16:16)

Jambo hilo litawageukia wale watakaokusanyika hapo:

14 Hawa watafanya vita na Mwana-Kondoo,na Mwana Kondoo atawashinda,kwa maana yeye ni Bwana wa Mabwana,na Mfalme wa Wafalme,na hao walio pamoja naye ndio walioitwa,na wateule,na waaminifu. (Ufunuo 17:14)

44 Na katika siku za wafalme hao Mungu

wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele,wala watu wengine hawataachiwa enzi yake;bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu,nao utasimama milele na milele. (Danieli 2:44)

8 Na mataifa walikasirika,hasira yao nayo ikaja,na wakati ukaja wa kuhukumiwa waliokufa,na wa kuwapa thawabu yao watumwa wako manabii na watakatifu,na hao walichao jina lako,wadogo kwa wakubwa,na kwa kuwahiribu hao waharibuo nchi. (Ufunuo 11:18).

15 Na upanga mkali hutoka kinywani mwake ili awapige mataifa kwa huo.Nao atawachunga kwa fimbo ya chuma,naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi.16 Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake,MFALME WA WAFALME,NA BWANA WA MABWANA.17 Kisha nikaona malaika mmoja amesimama katika jua;akalia kwa sauti kuu,akiwaambia ndege wote warukao katikati ya mbingu,Njoni mkutane kwa karamu ya Mungu iliyo kuu;18 mpate kula nyama ya wafalme,na nyama ya majemedari,na nyama ya watu hodari,na nyama ya farasi na ya watu wawapandao,na nyama ya

watu wote,waungwana kwa watumwa,wadogo kwa wakubwa.19 Kisha nikamwona huyo mnyama,na wafalme wa nchi,na majeshi yao,wamekutana kufanya vita na yeye aketiye juu ya farasi yule,tena na majeshi yake.20 Yule mnyama akakamatwa,na yule nabii wa uongo pamoja naye,yeye aliyezifanya hizo ishara mbele yake,ambazo kwa hizo aliwadanganya watu wale walioipokea ile chapa ya huyo mnyama,nao walioisujudia sanamu yake;hao wawili wakatupwa wangali hai katika ile ziwa la moto liwakalo kwa kiberiti; 21 na wale waliosalia waliuawa kwa upanga wake yeye aliyeketi juu ya yule farasi,upanga utokao katika kinywa chake.Na ndege wote wakashiba kwa nyama zao.(Ufunuo 19:15-21)


Hata kama tunayaona majivuno na ishara za vita,na vingi vitakavyotokea,hatimaye vyote havitafaulu.

Twaweza kuwa katika wakati ambapo mpanda farasi wa pili ameanza kuendesha farasi.Matokeo ya uendeshaji wao yatazidi kuwa mabaya.


Atafuatwa na farasi mweusi anayeonyesha uhaba wa chakula.

Vitabu vya bure vya Kanisa la Mungu *Linaloendelea*


www.ccog.org/books




Christians: AMBASSADORS



Continuing History of the Church of God




Dating: A Key to Success in Marriage



Faith for Those God has Called and Chosen

SOMO LA BIBLIA



SOMO LA 19B: KWA NINI AGANO JIPYA?

Bob Thiel, Mhariri Mkuu

Imechapishwa na Kanisa la Mungu *Linaloendelea*

Utangilizi:Kozi hii inatokana kwa kiwango kikubwa na Kozi kwa Mawasiliano iliyohaririwa mwaka wa 1954, iliyoanza chini ya usimamizi ya hayati C. Paul Meredith kupitia Kanisa la Mungu la Redio. Baadhi ya maeneo yake yameboreshwa ili yaendane na karne ya 21 (japo mengi ya maandishi ya awali yamebaki yalivyoo).Kadhalika imeongezewa vifungu toka Maandiko Matakatiifu, pamoja na taarifa na maswali ambayo hayakuwemo katika kozi ya awali. Maandiko mengi ya Biblia mara nyingi yatoka kwa New King James Version, yanatumika kwa idhini. NKJ pia inatumika. Pia, tafsiri zilizoandikwa za Kikatoliki kama vile New Jerusalem Bible (NJB) wakati mwingine inatumika kama vile tafsiri zingine. Anayetafsiri pia hutumia NBT (Neno Biblia Takatiifu).

Kwa Nini Agano JIPYA Linahitajika!

1. Je,Kristo aliyekuwa Mungu wa “Agano la Kale,” aliahidi kwamba atafanya Agano JIPYA-YAANI MAELEWANO MAPYA YA NDOA-na Israeli na Yuda hata baada ya Israeli wa Agano la Kale kufanywa mateka kwa kutotii Amri zake? Yeremia 31:31. Je,Waebrania 8:8 pia inathibitisha jambo hili?

MAONI: Kumbuka kwamba Agano Jipya bado lilikuwa

la SIKU ZA USONI wakati Paulo alikuwa akiandika Kitabu cha Waebrania.

2. Je,kuna sababu kwamba Agano Jipya ni lazima kwa hakika kwamba lile la kwanza lilikuwa na KASORO? Waebrania 8:7.
3. Kasoro ilikuwa wapi-Je! Ilikuwa kasoro ya Amri? Zaburi 19:7 na Warumi 7:12. Kwa vile kasoro HAIKUWA katika Amri,ambayo ni “kamilifu,”na siyo Mungu ambaye angetekeleza sehemu yake ya Agano,je,kasoro ilikuwa ni “yao”-yaani watu? Waebrania 8:8. Tazama mistari mitano ama maneno saba ya mwisho.

MAONI: Torati ni KAMILIFU. Lakini WATU walikuwa WADHAIFU – Wadhaifu KIROHO! Kwa hivyo,HAWAKUTUNZA SEHEMU YAO YA AGANO LA KALE AMBAYO NI MAELEWANO YA NDOA. Na pia,Agano la kale lilifanyiwa watu wanaokufa ambao wanaweza kufanya makosa,basi kukawa na agano la pili.

Lakini katika istilahi za Agano JIPYA ,Mungu anatarajia kufanya nini? Waebrania 8:10; Yeremia 31:33 na 2 Wakorintho 3:3-6.

Tazama NLT (New Living Translation) ya 2 Wakorintho 3:3-6:

3 mnadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo tuliyoikatibu,iliyoandikwa si kwa wino,bali kwa Roho wa Mungu aliye hai;si kwa vibao vya mawe,ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama.4 Na tumaini hilo tunalo mbele za Mungu kwa njia ya Kristo.5 Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lo lote kwamba ni letu wenyewe,bali utoshelevu wetu watoka kwa Mungu.6 Naye ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa agano jipya;si wa andiko,bali wa roho;kwa maana andiko huua,bali roho huhuisha . (2 Wakorintho 3:3-6, NLT)

MAONI: Chini ya agano la ndoa,Mungu aliandika sheria kwenye vibao viwili vya JIWE. Watu WANGEONA sheria kwa MACHO yao,lakini SHERIA HAIKUWA NDANI YA MIOYO NA MAWAZO YAO. Sheria haikuwa na SEHEMU yao. Lakini chini ya istilahi za agano jipya, Kristo aliahidi kwamba atafanya maelewano ya ndoa ya wale tu ambao SASA wana kanuni za Amri katika zilizoandikwa mioyoni mwao na mawazo yao na Roho

Mtakatifu.

KUMBUKA JAMBO HILI, KWA SABABU NI LA MUHIMU SANA!! Kristo ataoa “Bi harusi” – ambao ni washirika wa Kanisa lake kwa jumla– ikiwa wamejiweka tayari kwa KUJARIBU KUZITII amri zake.

Kulingana na masharti ya agano jipya la ndoa, lazima tujaribiwe na kuthibitishwa ikiwa twaweza kumtii Mungu kwa hakika. Kumbuka kwamba agano la kale lilitengenezwa na Waisraeli KABLA hawajajaribiwa na kupimwa. Agano jipya la ndoa halitafanywa HADI tujaribiwe na kupimwa na “kuzaliwa mara ya pili.” Baadaye tutakuwa washirika wa Ufalme wa Mungu wa KIROHO-Waisraeli kulingana na ROHO, na hatutakuwa tena na nia ile ya binadamu inayotenda dhambi.

Agano Jipya ni Agano BORA kuliko Agano la Kale. Agano la KALE lilikuwa ya KITAIFA-LA TAIFA MOJA PEKEE-yaani Israeli. Liliahidi BARAKA YA MALI YA KAWAIDA YASIYODUMU YA DUNIA. HALIKUWA NA AHADI YA ROHO MTAKATIFU NA UZIMA WA MILELE. Waisraeli wa Agano la Kale hawakuwa na ahadi ya kupokea Roho Mtakatifu ambaye angeandika amri za Mungu ndani ya mioyo yao.

Lakini makubaliano ya ndoa ya Agano JIPYA ambayo tutayaingia ndani yake yataleta SULUHISHO KAMILI litakalokebisha kosa la Agano la Kale na kulifanya rahisi kwa sisi kuzitii amri za Mungu KAMILI katika kusudi lake la kiroho! Kwa sababu katika ufufuo wa wafu, Kanisa lililozaliwa na Kristo litapewa asili MPYA kabisa-asili ya Mungu ya KIROHO-ambayo itawezesha Wakristo waliozaliwa mara ya pili kumtii KAMILI milele!(1 Yohana 3:9.) Baadaye Kristo ataoa Kanisa lake LINALOTII KAMILI.

Masharti ya Agano Jipya

1. Je, “Bwana” ndiye MJUMBE aliyekuja kupigia mbiu masharti ya Agano Jipya? Malaki 3:1, sehemu ya mwisho. Je, huyu mjumbe alikuwa YESU KRISTO? Marko 1:14.
2. Je, ujumbe wa Agano Jipya kawaida ni sehemu ya UJUMBE WA INJILI—habari njema—Kristo alihubiri? Marko 1:1, 14, 15. Je, toba na kuamini katika Injili ni mojawapo ya vitu ambavyo Waisraeli wa kisasa wanapaswa kufanya ili wapate kuingia katika Agano Jipya na Kristo? Mstari wa 15. Je, Mathayo 15:24 inathibitisha kwamba Kristo alitumwa kwa

“KONDOO” au watu WALIOTAWANYIKA wa wana wa ISRAELI kuitangaza Injili ya Ufalme? Je, Kristo BAADAYE aliwaamuru WANAFUNZI wake kuihubiri Injili – ambaye ina ujumbe wa Agano JIPYA-kwa ULIMWENGU WOTE? Mathayo 24:14 na 28:19-20.

3. Je, Mataifa sasa wana tumaini lo lote la kuwa warithi wa ahadi za maagano – yaani ahadi zilizokuwa katika maagano yaliyofanywa na Ibrahimu na ahadi za Agano Jipya? Waefeso 2:11, 12. Ni kwa njia gani mtu wa Mataifa-ambaye hana ukoo wa damu ya Ibrahimu-anaweza kuingia katika uhusiano wa Agano Jipya? Waebrania 2:13; Wagalatia 3:29 na Warumi 11:13, 17, 25.

MAONI: Katika masomo yaliyopita tulifundishwa jinsi mtu wa Mataifa anaweza kuingia katika uhusiano wa Agano Jipya: “Na KAMA ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na WARITHI sawasawa wa ahadi” (Wagalatia 3:29). Kwa hivyo Agano Jipya limefunguliwa kwa watu WOTE wa ulimwengu.

Kumbuka kwamba Agano Jipya lina MASHARTI – “ikiwa/kama.” Waisraeli na watu wa Mataifa lazima WAJITOE WENYEWU kwa Kristo na kujifunza KUMTII MUNGU (2 Wakorintho 3:2-3).

Lakini ndoa ya Agano Jipya, TOFAUTI na lile la kwanza, IMETANGULIZWA na WASIA-ambayo ni WOSIA.

4. Je, Yesu aliacha “agano,” ama WASIA wakati alifariki? Waebrania 9:15-17, KJV. Wasia wa Kristo ilikuwa na kusudi gani?

MAONI: Kama vile tulivyojifunza katika Somo la 18, AGANO NI WASIA-inatangaza MATAKWA ya mtu kwa utoaji wa MILKI zake baada ya KIFO chake .

Kristo aliacha wasia-AGANO-ambayo kila mtu angekuwa mfadhiliwa wa urithi wa milki zake. Kwa sababu mbegu MOJA –yaani Kristo –ndiye alipewa dunia kuwa urithi wake wa milele (Mwanzo 22:18; Wagalatia 3:16-19).

Kristo peke ndiye aliyezitii amri za Mungu kamili kwa hivyo anaweza kudai dunia kama urithi wake. Kwa hivyo yeye ndiye angeacha AGANO au WASIA wakati wa kifo chake ili kwamba “warithi” wake (Wagalatia 3:29) wapate kupokea kupitia kwake, urithi wa milele wa dunia.

Kumbuka kwamba AGANO jipya ama WASIA wa Yesu Kristo umekuwa ukifanya kazi tangia kifo chake. Lakini agano lake ama wasia wake una MASHARTI ambayo lazima tuyakidhi KABLA ya kurithi ahadi.

Neno la Kiyunani la “ agano” linamaanisha “ahadi.” Kwa vile AGANO jipya linahusisha makubaliano ya kutimiza masharti, linakuwa pia AHADI-na hiyo ahadi mpya haitathibitishwa ama kuanzishwa pamoja nasi-hatutaweza KURITHI ahadi ya urithi wa milele wa dunia na kuwa wana katika Ufalme wa Mungu wa kiroho utakaotawala-HADI tubadilishwe kuwa wenye MIILI ISIYOKUFA na kuwa na asili ya Mungu ili TUSIWEZE KUFANYA DHAMBI TENA! (2 Petro 1:4; 1 Yohana 3:9.)

Hebu tutazame neno la Kiyunani lililofasiriwa kama agano:

Msamiaji :: Kitabu cha Strong G1242 - diathēkē

Biblia ya KJV inatafsiri Strong G1242 kwa jinsi ifuatayo: ahadi (20x), agano (13x).

I. mwelekeo, mpangilio, ya namna fulani, ambayo mtu anahitaji kuwa sahihi, mwelekeo wa mwisho alioiweka wa kumiliki milki zake za kidunia baada ya kifo chake, agano au wasia

II. kilichofungwa, ahadi, agano

A. Ahadi ya Mungu kwa Nuhu, nk.

<https://www.blueletterbible.org/lang/lexicon/lexicon.cfm?Strong=G1242&t=KJV>

Kama kungekuwa na swala la kifo kwa mmoja wa waliofanya ahadi na hawakuingia katika maelewano basi ingekuwa kama WASIA-AGANO. Agano la kwanza lilikuwa tu kama MAELEWANO – “Utafanya hivi nami nitafanya vile.”

Sehemu ya pili ya Biblia basi ingekuwa na mada “AHADI MPYA” – MAELEWANO MAPYA – kwa sababu inadhihirisha kabisa AGANO JIPYA ambalo Mungu aliwatolea ukoo wa Israeli, na kwa watu WOTE wa dunia kupitia kwa Kristo.

Pia, sehemu ya mwisho ya Biblia ingekuwa na mada “AGANO,” kwa sababu “tukiwa wa Kristo, basi tumekuwa [kulingana na] mbegu ya Ibrahimu na [kupitia kwa KIFO cha Kristo] WARITHI wa ahadi” ambazo ZITAKAZOFAHAMIKA na Agano Jipya.

KWA HIVYO sehemu ya pili ya Biblia ingekuwa na mada, “AHADI MPYA NA AGANO JIPYA.” Lugha ya Kiyunani ambayo sehemu ya mwisho ya Biblia imeandikwa awali iliandikwa, inatumia lahaja ya Kiyunani “Diatheke” ambalo limetafasiriwa kama “AHADI” NA “AGANO.”

Agano Jipya Halijakamilishwa

1. Je! Yesu Kristo ni mhudumu wa Agano Jipya ? Waebrania 8:6. Je, Yesu ATA KAMILISHA kazi ya kuthibitisha Agano Jipya siku za usoni? Mstari huo . Pia, Waebrania 8:10 na Yeremia 31:31-34.

MAONI: “Siku” katika unabii wa Danieli 9:27 inawakilisha mwaka (Hesabu 14:34; Ezekieli 4:3-6).

Hayati Mwinjilisti wa Kanisa la Mungu Dkt. Herman Hoeh alisema:

Agano Jipya si maelezo mapya ya sheria. Kuna watu wengine ambao wanadhani kwamba kwa namna fulani Mathayo, Marko, Luka, Yohana, Matendo, na Barua za Paulo, Barua za Yohana, Petro, Yakobo, Yuda, na Ufunuo vimekuwa na maelezo yaliyoandikwa kuhusu vile agano jipya linafaa kuwa. Kwamba masharti yote ya agano jipya yameandikwa hatua kwa hatua katika agano jipya . Hakuna kitu kama hicho. Hakuna fungu lo lote katika Agano Jipya ambalo limetoa hoja za sheria. Hoja ambayo inaeleza kwamba kuna jambo linapaswa kuandikwa kwa mioyo yetu na mawazo kwa namna ya agano . Kwa sababu kwa hakika agano halijaandikwa bado. Yeremia 31 inasema kwamba agano litafanywa pindi tu Kristo atakaporudi tena na Kristo kwa ukweli hajarudi. Yesu alitua swali hilo akiongea katika Mathayo 5:6-7. Akiongea moja kwa moja ili kutatua swali hilo, alisema kwamba tusitarajie kupata maelezo mapya ya sheria katika kile kinachoitwa Agano Jipya . Badala ya hiyo, rudi nyuma ukatazame kile tunacho katika Agano la Kale ya Kiebrania. Unayo tafsiri kwa lugha ya Kiingereza ama kwa lugha yo yote vile ambayo unaisoma. Na uitazame. Na unaweza kutathmini. Na unaweza kutathmini kulingana na mifano nimeweka. Unaweza kuifunga mianya. Na unaweza kuinua mizigo yo yote. Na Yesu alieleza katika Mathayo 5 jinsi unaweza kuifunga mianya. Jinsi ya kuitazama sheria kwa kioo na

kuiona sheria wazi wazi kuliko vile ulivyokuwa ukiiona. Kwa sababu umekuwa na nafasi ya kuwa na Roho wa Mungu ,unaweza kutazama sheria ya Mungu,yaani Amri Kumi,sheria ya raia ambayo Mungu aliiweka kupitia kwa Musa na unaweza kutazama lengo na kusudi lake. Na Yesu alisema kwamba kuna wengine wetu ambao wanaenda kuzitunza na kufundisha hata hoja ndogo za amri na kuna wengine ambao watapuuzia kuzitunza na kufundisha.

Kupitia kwa Yesu,WATU WOTE walioitwa sasa wanaweza kuingia katika Agano Jipya na kuwa WARITHI “kulingana na ahadi” ambayo Mungu alifanya na Ibrahimu(Wagalatia 3:29).

Wakati Yesu atakaporudi duniani,ATAKAMILISHA agano aliyofanya na Ibrahimu. Ibrahimu na mbegu zake za KIROHO kupitia kwa Kristo wataurithi ulimwengu na uzima wa milele. Yesu pia ATAWEKA IMARA agano aliyofanya na Kanisa lake la kiroho KABLA hajarudi KUOA KANISA!

Agano Jipya lilitabiri kwamba Masihi atatangaza Agano Jipya (Yeremia 31:31).

Agano Jipya linaonyesha uhusiano wa Yesu Kristo :

28 kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano,imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi. (Mathayo 26:28)

6 Naye ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa agano jipya;si wa andiko,bali wa roho;kwa maana andiko huua,bali roho huhuisha. (2 Wakorintho 3:6)

6 Lakini sasa amepata huduma iliyo bora zaidi,kwa kadiri alivyo mjumbe wa agano lililo bora,lililoamriwa juu ya ahadi zilizo bora.7 Maana kama lile la kwanza lingalikuwa halina upungufu,nafasi isingalitafutwa kwa lile la pili.8 Maana,awalaumapo,asema Angalia,siku zinakuja,asema Bwana,Nami nitawatimizia nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda agano jipya;9 Halitakuwa kama lile nililoagana na baba zao,Katika siku ile nilipowashika mikono yao niwatoe katika nchi ya Misri.Kwa sababu hawakudumu katika agano langu,Mimi nami sikuwajali asema Bwana.10 Maana hili ndilo agano nitakaloagana na nyumba ya Israeli.

Baada ya siku zile,asema Bwana;Nitawapa sheria zangu katika nia zao,Na katika mioyo yao nitaziandika;Nami nitakuwa Mungu kwao,Na watakuwa watu wangu. (Waebrania 8:6-10)

2. Je,Ufunuo 19:7-9 imeeleza utukufu wa NDOA ya Kristo, aliye“Mwana Kondoo,” kwa Kanisa lililosafishwa LISILOKUWA NA DHAMBI wakati atakaporudi ? Soma pia 2 Wakorintho 11:2.

MAONI: Wale wote watakozaliwa mara ya pili kama viumbe vya kiroho wakati Kristo atakaporudi mara ya pili,watakaribishwa KIRASMI kuingia katika uhusiano wa ndoa wa Agano Jipya pamoja naye kama mume wao.Hivyo ndivyo Kristo ATASIMAMISHWA au KUKAMILISHA Agano Jipya na wao.

Kristo ATAOA tena “Mke” wake!

Wengine wanaweza kuuliza, “Yesu Kristo atawezaje kuoza Kanisa la Agano Jipya ikiwa aliishaoa Israeli wa awali waliokuwa chini ya Agano la Kale?”

Ukweli ni kwamba Yesu Kristo hajafungwa na ndoa ya Israeli wa awali! Mkataba huo wa ndoa ulivunjwa! Yuko huru kuoza TENA kulingana na sheria zinazotawala ndoa.Tazama vile amekuwa huru.

1. Baada ya Waisraeli wa awali kukosa kuzitii sheria za Mungu na kuzifuata desturi ya wapagani na kuitumikia miungu ya uongo,je,Bwana aliwasihi kugeuka kutoka kwa njia zao za UZINIFU? Yeremia 3:14.Je,Mungu “aliwafukuza”-na KUWAPA TALAKA –Waisraeli kwa sababu ya dhambi zao? Isaya 50:1;Yeremia 3:6,8 na Isaya 59:1-2.

MAONI: Wakati wana wa Israeli walivunja agano la ndoa ya Mungu,hakika walikuwa wakizini “KIROHO.”Walifuata desturi za wapagani na kuabudu sanamu zao kipagani badala ya BWANA Kristo aliyekuwa “Mume” wao.

Kwa vile Mungu ni MTAKATIFU,hawezi “kuishi pamoja” na dhambi! Kwa hivyo ilimlazimu kutengana na “ mke” –yaani Waisraeli wa awali (Isaya 50:1)

Japo Mungu aliwapa Israeli cheti cha talaka kwa ajili ya dhambi zake,Mungu hata hivyo hakuwa huru “kuoa” tena kulingana na Sheria! Kwa sababu Mwenyezi alisema, “BADO,NIMEWAOA” (Yeremia 3:14).

BWANA-Yesu Kristo aliyekuwa mwanadamu wa Agano Jipya-alikuwa amefungwa na sehemu yake ya masharti ya mkataba wa ndoa.

Masharti haya,hata hivyo yalipungukiwa na KIFO! Kifo cha mmoja wa wale washirika wa agano la ndoa kinaweza kuutenga uhusiano wa ndoa-ndoa inafunga hadi kifo,kama vile tulivyosoma hapo kwa somo la awali.

Kifo cha Yesu Kristo mtini kule Golgotha kilimweka huru kutoka kwa mkataba wa ndoa wa Israeli wa awali. Kristo Bwana wa Agano la Kale-Mungu katika MWILI-alikufa! Sasa yuko huru kuoia "Israeli wa kiroho" aliyetubu na kusamehewa na kuwa huru kutoka kwa dhambi-yaani Kanisa la Agano Jipya LITAKALOZALIWA MARA YA PILI-atakaporudi!

2. Yesu ataoa nani atakaporudi? Ufunuo 19:7. Kumbuka maneno "mke wake."

MAONI: Yesu aliahidi kufanya AGANO JIPYA-MAELEWANO MAPYA YA NDOA-wakati atakaporudi. Mkataba mpya wa ndoa utafanyika na Israeli wa "kiroho"-Waisraeli na watu wa Mataifa-ambao wamezaliwa kwa Roho.

Wakati huu mke wake atakuwa mwaminifu.Kwa nini? Kwa sababu wakati wa ufufuo atakuwa amekuwa amezaliwa taifa kamilifu katika Ufalme wa Mungu. Atakapozaliwa na Mungu,asili yao mpya ya KIROHO na nguvu itawaweza kuzitunza sheria zake KIKAMILIFU-sheria zile zile ambazo bado ni sheria na masharti ya uelewano wa ndoa-Agano Jipya-ambalo Kristo atafanya na Kanisa lake la Kiroho!

Kristo Alikuwa ili Tuweze KUTUNZA Amri

Wengine wanaamini kwamba Kristo alikuwa "kuitangua au kufutilia mbali torati."

Watu wengi hawajui kabisa MAMBO MENGI MUHIMU wanaopaswa kuyajua. Wale ambao wamejiweka kuwa wahudumu hawajafundisha watu ukweli,ama hata hao wenyewe hawajui ukweli huo.

1. Je,Kristo alikuwa "kuitangua torati"-yaani "kusulubisha sheria kwa msalaba"? Kristo MWENYEWE alisemaje? Tunapaswa kujua KILICHOMFANYA kuja.Maneno yake yalikuwa

gani? Mathayo 5:17.Je,mstari wa 18 na 19 pia inaonyesha kwamba HAKUJA kuharibu amri? Ni vitu gani viwili Yesu anasema "hutegemea amri ZOTE"? Mathayo 22:40,37-39.

MAONI: Amri za Mungu za kifalme imekuwako tangia zamani. Amri hiyo,pamoja na hoja zake kumi-Amri Kumi-zimekuwa tangia wakati wa Bustani wa Edeni. Amri itasimama MILELE. Upendo wa Mungu kama ulivyodhihirishwa na amri yake haijawahi kuwa kuukuu (Zaburi 111:7, 8, KJV, NLT). Watu ndio wameshindwa kujileta katika maelewano na amri zilizo kuu!!

Kristo ANARUDIA mara mbili hapo kwa KUSISITIZA kwamba hakuja kuitangua –ama kuifutilia mbali-amri.

2. Kwa njia nyingine,je!Yesu alisema amekuwa KUFANYA nini? Mathayo 5:17,maneno tisa ya mwisho.Je!Yesu alimaanisha nini aliposema maneno "NIMEKUJA...KUTIMILIZA?" Tazama maoni.

MAONI: KRISTO "ALITIMILIZA TORATI" KAMILI KWA KUITII AMRI! Kwa dhahiri Kristo "alipotimiliza" amri HAKUFUTILIA MBALI TORATI! ALIONYESHA NGUVU ya Roho wa Mungu ambayo inawekwa ndani ya mtu kumwezesha kuitimiliza –kuitunza-sheria ya kiroho. Kwa sababu kwa Mungu CHOCHOTE chawezekana (Mathayo 19:26).

Wacha tutazame kwa ufupi neno la Kiyunani ambalo limefasiriwa kama kutimiliza:

Msamiati :: Kwa Kamusi ya Strong G4137 – plēroō

Mpangilio wa matumizi yake ya Kibiblia [?]

I. Kujaza hadi pomoni,kujaza hadi ijae,k.v kujaza hadi kifike juu.

A. Kuifanya iongezeke,kutoa au kusambaza

i. Nimezidisha,nimesambaza kwa uwingi

II. Kutoa kamili,k.v.Kukamilisha

Kujaza hadi juu:ili kwamba isibaki nafasi yo yote ya kuhitaji kujazwa,yaani kujaza pomoni.

A. kilichokamilika:nambari

Kukamilisha kwa njia yo yote,kuweka timilifu

i. Kuinua hadi mwisho,kutekeleza,kufanikisha (shughuli fulani)

B. Kuiweka ifanye kazi,Kuitambulisha,kutambua

Masuala ya kazi: kufanya, kutekeleza

i. Ya usemi, ahadi, unabii, kuitimiliza, kuidhinisha, kutekeleza

ii. kuitimiza, yaani kuiweka kwa mapenzi ya Mungu (kama vile ilivyofanywa kwa torati) kuitii kama ilivyokusudiwa, na ahadi za Mungu (zilizotolewa kupitia kwa manabii) ili zipate utimizaji

<https://www.blueletterbible.org/lang/lexicon/lexicon.cfm?Strong=G4137&t=KJV>

Kristo ndiye alikuwa mzaliwa wa kwanza kwa ndugu wengi. Alikuwa mwanadamu wa kawaida kama mimi na wewe lakini ALIZALIWA kwa Roho Mtakatifu wa Mungu katika mwili wa KAWAIDA, ambayo kwetu sisi, mimi na wewe tutazaliwa BAADAYE katika maisha-tukiwa tumetubu dhambi, na kukubali dhabihu ya Yesu kwa ajili ya dhambi zetu, na kubatizwa (Matendo 2:38).

Kristo alikuja kulipia gharama ya dhambi zetu kwa kutumia uhai wake, ambao ulikuwa ni MAUTI ya pili. Anatuwezesha tupokee Roho Mtakatifu wa NGUVU ambayo twaweza KUTIMILIZA AMRI pia, na hatimaye twaweza kuingia kwa uhusiano wa Agano JIPYA na yeye!

Ni nani Mungu anampa Roho Mtakatifu?

Wale WANAOMTII kulingana na Matendo 5:32.

Kwa kufunuliwa kwa ahadi ya Agano JIPYA la Roho ambayo ndiyo uwezo wa kuitunza Torati, Mungu sasa anaweza KUITUKUZA-KUPANUA-Amri zake kutoka kwa utunzaji wa kimmandiko, kama vile ilivyonenwa na Agano la KALE, hadi kwa lengo la awali la Mungu aliyoitaka kuanzia mwanzo katika Bustani ya Edeni.

Mungu SASA anaihitaji sisi kuitunza amri kwa ROHO-kwa madhumuni yake ya KIROHO. Hii HAIWEZEKANI kwa wanadamu walio na nia ya mwili PASI na Roho wa Mungu! Lakini wanadamu wanaweza kuwa na NGUVU ZA KIROHO za Roho Mtakatifu kuitekeleza tendo hili kubwa, IKIWA watajitoa kwa Mungu!

Kwa hivyo Kristo pia alikuja KUITUKUZA torati. Hiyo ndiyo maana alisema, "Mmesikia kwamba imenenwa [na wale waliotoa sheria chini ya Agano la KALE], Usizini (KIMWILI) lakini mimi nawaambia, Kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani [KWA

MAWAZO) AMEKWISHA kuzini naye moyoni mwake" (Mathayo 5:27-28). BASI inahesabiwa kama dhambi ikiwa mtu ataacha MAWAZO ya usinzi uingie katika akili yake, ama akianza kufanya matendo ya dhambi ya aina yo yote.

Katika njia hizi mbili, basi, Kristo alikuja "kutimiliza torati": YEYE mwenyewe alitimiliza Torati kwa KUZITII, na ameruhusu "ye yote atakayeweza" kutimiliza ama kutii katika ROHO na pia katika maandiko!

Katika Agano Jipya, twaona Yesu akifundisha kila Amri Kumi (tazama kitabu chetu cha mtandao wa intaneti ccog.org, The Ten Commandments: The Decalogue, Christianity, and the Beast)

Matayarisho Tunayopaswa Kufanya kama Bi Harusi Mtarajiwa

1. Je! Agano la Kale limekuwa na KUSUDI gani?

MAONI: Imekuwa ya maana sana Mungu AWAFAANYE WANADAMU, kupitia kwa uzoefu, WAGUNDUE kwa muda mrefu hakika kwamba raha ya kweli inapatikana tu kwa kuishi kulingana na amri za upendo na za milele za Mungu, na kufanya wanadamu wagundue kwamba kwa nguvu zao hawana uwezo.

Agano la KALE lilifanya jambo hilo! Kwa muda wa karne nyingi, wana wa Israeli wamejulikana kama taifa la Mungu. Japo twajua kwamba Israeli hawakutunza amri. Kwa hivyo, Israeli limekuwa mfano kwa ulimwengu kwamba binadamu ASILI hawezi kutunza sheria za Mungu kwa uwezo wake mwenyewe.

Lakini sasa Mungu amemtuma Mwana wake kwa ulimwengu huu unaotawaliwa na dhambi na umekosa raha na ujumbe mpya—"Habari Njema"- wa kuja kwa nguvu za kiroho na tangazo la Agano JIPYA. Agano la KUZALIWA tena, KUKUA tena, na kwa kurudi kwake Kristo KUZALIWA TENA-wakati huu atakuwa na nia TOFAUTI na MPYA-NIA YA KIROHO!

2. Kila mmoja wetu lazima apokee ROHO MTAKATIFU ambaye atafanya mabadiliko ambayo yatafanyika ndani yetu kabla " hatujazaliwa mara ya pili" katika mwili wa kiroho na ASILI TAKATIFU ya kiroho ambao lazima tuwe nao ili Kristo ASIMAMISHE

ahadi mpya ya ndoa na sisi.

Lakini masharti gani twapaswa kuyatimiliza kwa kina ili tuweze KUPOKEA Roho Mtakatifu atakayetusaidia kuleta haya mabadiliko? Ni nini Kristo anasema tufanye ili tuweze kupokea Roho Mtakatifu? Matendo 2:38 na 5:32.

MAONI: Hapa twapata kile kinachotakikana ili uwe mshirika wa Kanisa ambalo Kristo ataoa. Unapaswa kuyafanya mambo matatu SASA ILI UWEZE KUPOKEA ROHO MTAKATIFU ALIYEAHIDIWA ambaye anakuweka katika Kanisa lake (1 Wakorintho 12:13). LAZIMA UTUBU, UAMINI NA UBATIZWE!

Lakini haya yote yanamaanisha nini? Wacha tupate kuelewa:

KWANZA: Lazima "UTUBU"-kuvunjika kuhusu msamaha wa maisha ya DHAMBI na KUJISALIMISHA kwa UTAWALA WA UPENDO wa Mungu-kwa sababu Mungu hawezi kumwokoza ye yote ambaye hawezi kutawala.

Kristo ANAKOMBOA Wakristo wa kweli kupitia kwa damu yake iliyotiririka mtini kwa adhabu ya dhambi zao ili kwamba wasife kifo cha pili cha milele. Hiyo ina maana kwamba KRISTO ANAWAKOMBOA WALE AMBAO WAMEJITAYARISHA SASA KUIINGIA KATIKA AGANO JIPYA NAYE wakati wa kurudi kwake, na ameahidi sasa kuwapa Roho Mtakatifu aishi ndani yao.

Wale ambao wamekubali kuingia katika Agano Jipya na Kristo basi wanakubali kuwa WATUMISHI WALIOKOMBOLEWA-na kufanya "mapenzi yake"-tofauti na wale waliokuwa katika Agano la Kale – yaani wanafanya "kwa MOYO" (Waefeso 6:6). Kwa sababu Mungu atayaandika masharti ya Agano Jipya kwa "meza mpya ya moyo" (Yeremia 31:33 na Ezekieli 11:19-20), kwa kutumia Roho Mtakatifu aliye ndani yako! (2 Wakorintho 3:3).

PILI: Lazima uamini kwamba Kristo ndiye Mwokozi wako, na Kuhani Mkuu wako sasa, na Mtawala atakayekuja. Na lazima UAMINI kwamba atatuma Roho Mtakatifu mwenye NGUVU ili akusaidie KUVUNJA nia yako ya awali na KUKUBADILISHA.

Kristo, kwa kulipa gharama ya dhambi kwa uhai wake, ameleta uwezekano wa kila mtu kuingia

katika uzima wa MILELE. Ndiyo maana tukitazama KUSHINDWA kwa Waisraeli kutunza sheria chini ya Agano la Kale, twagundua kwamba tunamhitaji Mwokozi-Kristo-kutulipia dhambi na kutupatia nguvu zake. Tunagundua MASOMO ya Agano la Kale yamekuwa "kiongozi" wa kutuleta kwa Kristo (Wagalatia 3:24, KJV). Na hiyo ni nzuri kwa sababu twamkubali kama Mkombozi wetu, Mtawala na Mfalme na MUME wetu!

TATU: Lazima UBATIZWE.

Kwa MUHTASARI, LAZIMA: (1) utubu, (2) uamini, (3) ubatizwe.

BAADA ya kufanya hivyo, Mungu anaahidi kufanya nini kulingana na masharti ya Ahadi au Agano? "...nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu"!! (Matendo 2:38.) Hii ndiyo AHADI Mungu ametuahidi kama sehemu yake baada ya kufanya hayo.

Basi ndiyo hayo!

Hii ndiyo roho ya NGUVU iliyowajia mitume mara baada ya kifo cha Kristo (Matendo 2:4). Na HAYA ndiyo yanahitajika kabla ya kuingia katika uhusiano wa agano jipya na Kristo wakati wa ufufuo-wakati wa kurudi kwake. Na hapo ndipo tutakaporithi vitu vya ajabu ambavyo Agano Jipya linatuhidi-yaani uzima wa milele, kuwa wana katika ufalme wa Mungu, na dunia kama urithi wa MILELE.

Roho Mtakatifu anatupatia NGUVU tunayohitaji ili ATUANDAE SASA ILI tupokee Baraka hizi zote!

Uamuzi Ni Wako

Ikiwa unataka kuingia katika Agano Jipya la ndoa na Kristo, unapaswa kuanza MAANDALIZI SASA! Hapo baadaye utakuwa UMECHELEWA. Lakini kufanya uamuzi ni WAKO. Mungu hatakulazimisha. Anakuacha UICHAGUE MWENYEWE. Kumbuka:

1. Wakati Mungu alitoa Agano la Kale kwa Israeli wa awali, Je, aliwalazimisha kuingia katika agano naye, ama aliwaruhusu KUCHAGUA KWA HIARI ikiwa wataweza kuingia katika agano? Kutoka 19:3,5-8. Kumbuka neno "IKIWA" katika mstari wa 5.

MAONI: Neno "IKIWA" linaonyesha kwamba Mungu hakuwalazimisha Israeli wa awali kuingia katika Agano la Kale na yeye.

2. Je! Mungu aliwashurutisha kizazi KIJACHO cha Waisreali ,walioishi miaka arubaini baadaye ili kuingia katika Agano na yeye,ama aliwaruhusu KUCHAGUA kama ikiwa watafanya ama hawatafanya? Kumbukumbu 30:19.Kumbuka maneno "CHAGUA uzima."

MAONI: Kristo hatalazimisha mtu ye yote kuingia katika agano na yeye.Na pia hatakulazimisha kufanya uamuzi wa KUANZA KUJIANDAA kuingia katika Agano Jipya naye atakaporudi.Kwa nini?

Mungu aliumba binadamu na uwezo kama yake-viumbe wenye MAWAZO kama yake,hata kama ana upungufu-wanadamu ni viumbe ambavyo wanaweza KUCHAGUA-wanadamu ni WAKALA WALIO NA UHURU,na pia sio vyombo vinavyoendeshwa tu kama viumbe vingine.

Kristo HAKUMLAZIMU mtu ye yote kufanya agano na yeye,na hataweza kufanya hivyo! Kwa sababu yuko kwa mchakato wa kutayarisha wanadamu ambao WANAJIFUNZA KUCHAGUA VILIVYO! Wao ndio watakaokuwa UUMBAJI WA WAKUU WA MUNGU WA KIROHO!

Mungu atatoa ushauri na kusema, "chagua UZIMA." Na WEWE ni wakala huru kama wale wa vizazi vya awali ambao agano jingine,lile la Kale walipewa.Na wewe utachagua nini?

Agano Jipya linaahidi uzima-yaani Uzima wa MILELE-na uhusiano wa karibu na Kristo kama Bwana haruswa wote.Na pia mibaraka yote itakayofikia wale walioitwa wito mkuu.

Wewe utafanyaje SASA kuhusu Agano Jipya ambalo litatolewa na Kristo wakati wa kurudi kwake? Ikiwa UTAKATAA KUCHAGUA kujiandaa sasa kwa kuingia katika Agano kwa kukataa kumruhusu Mungu kuweka ROHO wa uzima wa milele ndani yako,hautabadilishwa kuwa kiumbe kama roho atakaporudi Kristo hivi karibuni.

Mungu hatafanya na wewe agano JIPYA la ndoa ikiwa umebaki MWANADAMU.Ili uhudhuri sherehe ya haruswa ya Mwana Kondoo,lazima "uzaliwe mara ya pili" kama ROHO-vile Mungu alivyo!

Kuzidi kukataa kumtii Mungu na kuanza kuandaa kunaweza kuleta MAUTI YA MILELE!

Wakati umefika SASA ya kufanya uamuzi.WAZA KWA KINA kwa suala hili ukita fakari somo hili na masomo mengine yanayokuja mbeleni.Haya yatazidi kukupa maagizo ya Mungu yanayofunuliwa JINSI UNEWEZA kuingia katika Agano Jipya,yaani uhusiano wa BWANA-na BI HARUSI na Yesu Kristo aliye hai,ambaye ni Mkombozi wako.

Mungu Anafanya Kazi Kupitia kwa Kanisa Lake

Uthibitisho umekuwa wazi kwamba ili upate KUURITHI uzima wa milele lazima uwe tayari kuingia katika uhusiano wa Agano Jipya na Kristo.Hiyo ndiyo njia pekee ya kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu wa Mungu aliye hai,na kurithi ahadi ya Mungu.

Lakini ni nani atakupatia ushauri katika kujiandaa sasa ili uwe tayari kuingia katika ndoa ya Agano Jipya na Kristo atakaporudi kwa ghafula? Je! Mungu analo KANISA duniani leo ambalo linaweza kuupokea ushauri wa kipekee?Ama unadhani kwamba unaweza kuingia katika uhusiano wa Agano Jipya na Kristo ukihudhuria kanisa Lolote?

Je! Mungu amekuacha kwa giza kuhusu maarifa haya ya muhimu? Ama anakuonyesha uhakika kwamba kuna Kanisa,na kukuonyesha jinsi yaKUTAMBUA Kanisa hilo kati ya makanisa na madhehebu 450 yaliyo ulimwenguni leo?

Kanisa GANI?-hilo ni swali la muhimu linalojumuisha! Biblia inatoa jawabu la swali hili pia.Wacha tuelewe vile Biblia inavyosema.

1. Hapo zamani kabla Musa na Sinai,Je! Mungu alikuwa na KUHANI duniani ambaye ALIMWAKILISHA,na kufanya kazi yake? Mwanzo 14:18-19.Pia rejelea Somo la 7,Kumaliza Shida ya Fedha,kutoka swali la 5 kuendelea.
2. Je! Baadaye Mungu alimwita Musa kuwa MTUMISHI wake? Kutoka 3:11-12.Je! Mungu alimtumia MUSA kutoa masharti ya Agano la Kale kwa Waisraeli juu ya Mlima Sinai? Kutoka 19:3-8;21:1 na 24:3.
3. Je,alikuwa MTU ALIYE NA MWILI USIODUMU-MWANADAMU ALIYE NA DAMU-Yesu Kristo (Waebrania 2:9,14)- alikuja kutangazia Mungu masharti ya Agano Jipya kwa watu wa wakati

wake na kwa ulimwengu? Malaki 3:1 na Marko 1:14.

MAONI: Mungu hutumia WANADAMU kumwakilisha katika kufanya shughuli zake za kidini na wanadamu wengine hapa duniani. Baada ya Mungu kuwapa watu Amri Kumi kwenye Mlima wa Sinai, ni MWANADAMU, Musa ambaye alitoa masharti ya Agano la Kale kwa watu wa Mungu. Baadaye Mungu alitumia Kristo, katika umbo la MWANADAMU, kutangaza masharti ya Agano Jipya. Na LEO HII Mungu anatumia wanadamu wengine kumwakilisha katika kushughulikia wanadamu (tazama Waefeso 4:7-16; 1 Wakorintho 12:12-13).

Injili ni ujumbe kuhusu UFALME wa Mungu unaokuja kusimamishwa hapa duniani. Ujumbe wa injili ni pamoja na UJUMBE WA AGANO JIPYA ambao watu "watakozaliwa mara ya pili" wataagana na Kristo ili wapate kutawala ulimwengu na yeye katika uhusiano wa mume na mke siku za usoni, yaani Ufalme wa Mungu unaotawaliwa kiroho.

4. Kristo mwenyewe alikuwa hapa duniani lakini kwa muda mfupi. Ni ukweli kwamba KRISTO ALIANZISHA KANISA KUUENEZA UJUMBE WA AGANO JIPYA KWA WATU WA VIZAZI VYOTE ILI wapokee Roho Mtakatifu na basi wajitayarisha kuingia katika Ufalme wakati atakaporudi upesi? Mathayo 16:18.

5. Je! Hili Kanisa lingekuwa na madhehebu mengi TOFAUTI? Ama lingekuwa KANISA MOJA? Mstari huo. Je, Kanisa hilo la kweli lingekuwa na "funguo" za Ufalme-yaani maarifa ya JINSI ya KUIINGIA katika Ufalme wa Mungu? Mstari wa 19.

MAONI: Moja ya FUNGUO HIZO MUHIMU ni kujua kwamba KUNA Agano Jipya na kujua jinsi ya kuingia katika Agano hilo-kujua KUSHIKA SEHEMU YAKO ili kwamba Mungu azidi kukamilisha sehemu yake. Kanisa ambalo unapaswa kuwa ni lile ambalo lina ufunguo huu muhimu!

6. Baada ya Agano Jipya kujulikana, Roho Mtakatifu ALIYEAHIDIWA alipata kuingia siku gani ndani ya wale ambao walijua kupokea karama za Roho Mtakatifu? Matendo 1:4,5; 2:1-4. Kwa kuingia kwa Roho Mtakatifu ndani ya watu hawa-na kuzaliwa na Mungu kiroho-je! WALIINGIZWA NDANI YA "MWILI" WA KRISTO-ambalo ni Kanisa la Mungu?

I Wakorintho 12:12-13.

MAONI: Hawa watu, kwa kutoa mapenzi yao kwa Mungu, na kwa kuwa na Roho Mtakatifu ndani yao, walipata kuwa WASHIRIKA wa mwili wa kiroho-yaani Kanisa la Mungu. Walipata kuwa washirika wa mwili kama vile viungo vya mwili kama-masikio, mikono, miguu-ni washirika au viungo vya mwili na vilivyo chini yake. Hii ndiyo asili ya KANISA LA KWANZA LA MUNGU LA KIROHO DUNIANI!

7. Je! Maandiko yafuatayo yanaonyesha wazi kwamba Kanisa la Mungu la KWELI linafaa kuwa na jina "KANISA LA MUNGU"? Soma na uandike THIBITISHO HIZI MUHIMU: Matendo 20:28; 1 Wakorintho 1:2,10; 32,11:22,15:9; 2 Wakorintho 1:1; 1 Wathesalonike 2:14; 2 Wathesalonike 1:4; 1 Timotheo 3:5 na Wagalatia 1:113.

8. Kupitia kwa awamu yote ya maisha, tangia wakati wa Kristo, je! Kumekuwako kundi dogo ambalo limeendelea kama watekelezaji na wasimamizi wa vitu vinavyohusu Agano Jipya na mapenzi ya Mungu? Ufunuo 1:20; 2:1,8,12,18; 3:1,7.

MAONI: Haya Makanisa saba yaliyotajwa hapa yalikuwepo wakati wa mitume. Lakini pia yanaonyesha awamu ya Kanisa la Mungu la kweli katika hatua zinazofuatana kuanzia wakati wa mitume hadi leo. Makanisa haya yanaweza kufuatiliwa kupitia kwa historia!

Sisi tulio katika Kanisa la Mungu Linaloendelea twajua kwamba sisi ni wazao wa kiroho wa Waefeso na Wasmirna (na pia waumini wa awali waliokuwa Antiokia) na pia twaweza kupata rekodi ya mafuatano ya viongozi toka karne ya kwanza hadi mwanzo wa karne ya 3. Sisi katika Kanisa la Mungu Linaloendelea pia twajua kwamba tunawakilisha mabakio ya waumini waaminifu sana wa awamu ya Kanisa la Mungu la Filadelfia linaloendelea kwa wakati huu (Waebrania 13:1; Ufunuo 3:7-13).

Ni Kanisa la kweli la Mungu ndilo lina aina ya mfuatano wa kiroho na uendelezaji wa imani ya awali ya mitume ambayo wale wanaohusiana na imani ya Wakatoliki na Othodoksi ya Mashariki wanadai kuwa nayo. (Uhakikishe umeshusha nakala yako ya bure ya kitabu KINACHOFUNUA kuhusu historia ya Kanisa linaloendelea "Continuing History of the Church of God" kwa www.ccog.org)

Kanisa la Mungu Linaloendelea

Kutangaza Injili ya Ufalme wa Mungu (Mathayo 24:14) pamoja na kufundisha yale yote Yesu aliamuru (Mathayo 28:19-20) ndiyo tume kubwa ya Kanisa la Mungu leo. Ujumbe wa Injili unafaa kupelekwa kwa kila pembe za dunia kabla Kristo hajarudi.

WOKOVU unakuja tu kwa njia ya Mungu (Matendo 4:12;16:31;Zaburi 62:1;2 Timotheo 1:9). Na anatumia Kanisa lake-Kanisa ambalo Roho anapatikana ndani yake-kuhubiri injili hiyo zaidi (Warumi 10:14-15).

Kama vile masharti ya Agano Jipya ni sehemu ya Ahadi ya Mwokozi au WASIA, Kanisa la Mungu la kweli leo hii linasaidia MTEKELEZAJI AU MSIMAMIZI wa wasia hii ambayo kwayo twawezapata Roho Mtakatifu ili tupate kuingia katika Ufalme wa Mungu.

Hakika kwamba Kanisa la Mungu linajua kwa NINI Wasia hii ilitengenezwa-lengo KAMILI na kusudi lake-pamoja na thibitisho kwamba ni Kanisa la Mungu la KWELI lililoanzishwa kutekeleza Wasia, linafanya wahudumu wake wawe watekelezaji! Kristo aliwapa mitume wake funguo za UFAHAMU wa kweli, ambao unafungua mlango wa UFALME WA MUNGU (Mathayo 16:19).

Kanisa la Mungu la kweli si aina ya kanisa la "kipentecoste" linalopiga kelele isiyo ya maana. Roho wa Mungu ni Roho ya kiasi" (1 Wakorintho 14:33;2 Timotheo 1:7), ni Kanisa la kiasi ambalo lina uelewa wa kweli wa Ufalme.

1. Kuna Roho wa PEKEE katika Kanisa la Mungu-Roho MTAKATIFU wa Mungu. Kwa Roho huyu twapata kubatizwa kwa Kanisa LAKE. Lakini Je, Paulo AMEKUONYA kuhusu kupokea "roho" TOFAUTI? 2 Wakorintho 11:4.

MAONI: Roho hii TOFAUTI ni roho ya "Mpinga Kristo" (1 Yohana 2:18,4:3). Roho hii INAPINGA Kristo. Ingawa makundi katika MADHEHEBU. Siyo Roho Mtakatifu wa Mungu anayeunganisha.

Usifanye kosa la kujaribu kufanya AGANO na Mungu kupitia kwa Kanisa la UWONGO. Ukifanya hivyo, mtume Yohana anakuonya hapa kwamba utapokea ROHO YA UWONGO. Utapata kwamba unaongozwa kwa kutoshika amri za Mungu kama ilivyoamriwa na Mungu na kufunuliwa kwa neno Lake, ambalo ni Biblia.

2. Je! Kuna maonyo mengine yaliyotolewa dhidi ya kufanya agano na Mungu kupitia makanisa ya uwongo? Marko 13:6.

MAONI: Sio wachache, lakini WENGI-watakuja kwa jina la Kristo, na kujihesabu KIMAKOSA kama WAKRISTO, na WATADANGANYA WENGI!

Kumbuka kwamba baada ya wewe kuzaliwa kwa Roho Mtakatifu, lazima UKUE KIROHO. Ukichagua kanisa baya kupitia kwa agano na Mungu, utalishwa na chakula kibaya kiroho. Utaweza kunyauka na KUFA KIROHO ukipewa chakula cha kiroho kisichofaa-kwa sababu ni sumu! Elewa kwamba Kanisa la kweli la Wakristo SI Protestani (tazama kitabu chetu cha mtandao, Hope of Salvation: How the Continuing Church of God Differs from Protestantism) na pia sio Katoliki wa Ugiriki-Rumi (tazama kitabu chetu cha mtandao, Beliefs of the Original Catholic Church). Hatimaye, ujue kwamba UJUMBE WA ONYO LA MWISHO UTAFIKIA DUNIA NZIMA. Sisi katika Kanisa la Mungu Linaloendelea tunatumia teknolojia ya kisasa kufanya kazi ya kutekeleza Mathayo 24:14, Mathayo 28:19-20 na Warumi 11:25 pamoja na kujiandaa kwa kazi fupi ya Warumi 9:28. Tunagundua kwamba awamu ya mwisho wa kazi ina sehemu nyingi, lakini tunaongoza kwa ile tunaweza.

Tumeweza kufikia mamilioni kumi ya watu katika nchi na himaya 220 kupitia kwa intaneti, runinga ya mtandao, redio, kuandikia watu, na kuchapisha neno.

Makanisa mengine ya Waprotestani ya Ugiriki –Rumi WAMETUMIA KWA NJIA ISIYO HALALI jina la Kanisa la Mungu la kweli "yaani Kanisa la Mungu," kama vile walivyotumia VIBAYA Jina la Kristo wakisema ni Wakristo.

Masalio ya Wanafiladelfia wanaofanya kazi kwa uaminifu duniani ni Kanisa la Mungu Linaloendelea, ambalo lina makao makuu na anwani ni: 1036W. Grand Avenue, Grover Beach, CA 93433 (Marekani).

Kumbuka kweli hizi ukiendelea kusoma zaidi, kwa masomo yatakayokuja mbele kuhusu kuingia katika Agano Jipya na Yesu Kristo atakaporudi mara ya pili!

Kumbuka, ikiwa unaitwa na Mungu, uamuzi kuingia katika Agano la Mungu ni JUU YAKO!

Kwa Nini Mungu Anaruhusu Mateso?

Hiki ni kitabu chetu cha mtandao wa tovuti ccog.org, ambacho kinaitwa *Siri ya Mpango wa Mungu*:

Ikiwa Yesu alikuja ili tupate uzima “tele” (Yohana 10:10), je! Mungu bado anaruhusu mateso?

Ndiyo.

Je, kuna kusudi la mateso tunayopata?

Ndiyo.

31. Kwa kuwa Bwana hatamtupa mtu hata milele. 32 Maana hajapomhuzunisha, atamrehemu, kwa kadiri ya wingi wa huruma zake. 33 Maana moyo wako hapendi kuwatesa wanadamu. Wala kuwahuzunisha. (Maombolezo 3:31-33)

Kumbuka kwamba Mungu hapendi kututesa au kutuhuzunisha. Anataka tufanikiwe (3 Yohana 2).

Inaonekana kwamba mambo mabaya yanapata watu wazuri.


Yesu hakutenda dhambi (Waebrania 4:15), lakini aliteswa kwa ajili yetu (1 Petro 2:21). Na “ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata (Waebrania 5:8)

Kwa nini Mungu anaruhusu wanadamu kuteseka?

Kuna sababu nyingi za kuteseka. Mojawapo ni kutuadhibu kwa sababu ya matokeo ya dhambi ili tuhimizwe tusitende dhambi na kumrudia Mungu (Maombolezo 3:39-40; Walawi 26:18). Na tunapaswa kuelewa kwamba Biblia inafundisha kuwa Mungu anatuadhibu kwa njia isiyostahili maovu yetu (Ezra 9:13; Ayubu 11:6). Basi, hata watu ambao wanaamini kidogo katika sehemu hizo za Biblia, wanagundua kwamba Mungu anatuadhibu kiasi tu.

Lakini kuna sababu nyingine ambayo inatatiza sana.

Mtume Paulo anatueleza kwamba “Kwa maana viumbe vyote pia vilitiishwa chini ya ubatili, si kwa



hiari yake, ila kwa sababu yake yeye aliyeviitisha katika tumaini” (Warumi 8:20). Pia aliandika:

16 Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku. 17 Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo wa muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; 18 tusivingalie vinavyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda; bali visivyoonekana ni vya milele. (2 Wakorintho 4:16-18)

Watu wako kwa harakati ya kusafishwa – ambayo ni pamoja na huzuni na mateso – japo kuna tumaini. Wale hawajaitwa katika kipindi hiki wanasafishwa kwa njia moja (Isaya 48:10; Yereimia 9:7), na wale walioitwa watakaswa na kusafishwa kama fedha au dhahabu (Zekaria 13:9; Zaburi 66:10; Danieli 11:35, 12:10; 1 Petro 1:7; Ufunuo 3:18). Kwa hivyo kuna majaribu kama “moto” katika awamu hii (1 Petro 1:7; 4:12).

Hili ni tumaini kwa kile kitakachokuwa bora:

9 Lakini, wapenzi, ijapokuwa twanena hayo, katika habari zenu tumesadiki mambo yaliyo mazuri zaidi, na yaliyo na wokovu. 10 Maana Mungu si dhalimu hata iasahau kazi yenu, na pendo lile mlilolidhihirisha kwa jina lake, kwa kuwa mmewahudumia watakatifu, na hata sasa mngali mkiwahudumia. 11 Nasi twataka sana kila mmoja wenu aidhihirishe bidii ile ile, kwa utimilifu wa matumaini hata mwisho; 12 ili msiwe wavivu, bali mkawe wafuasi wa hao wazirithio ahadi kwa imani na utimilivu. (Waebrania 6:9-12)

Kwa hivyo, Twapaswa kuwa na subira na ujasiri kwamba njia za Mungu zitaleta “vitu vizuri.”

Wakati mwingine watu huteseka kwa kufanya mema:

17 Maana ni afadhali kuteswa kwa kutenda mema, ikiwa ndiyo mapenzi ya Mungu. (1 Petro 3:17)

Kumbuka kwamba maneno hayo HAYASEMI kwamba ni mapenzi ya Mungu kuleta mateso ili kwamba tuwe duni.

Basi,Biblia ni wazi kwamba kuna faida ambazo zitatokea kwa mateso ambayo yanatupata:

3 Huzuni ni afadhali kuliko kicheko, Maana simanzi ya uso ni faida ya moyo. 4 Moyo wake mwenye hekima umo nyumbani mwa matanga, bali wake mpumbavu umo nyumbani mwa furaha. (Mhubiri 7:3-4)

16 Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu; 17 na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye. (Warumi 8:16-17, AFV)

18 Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu. (Warumi 8:18)

12 Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho. 13 Lakini kama mnavyoshiriki mateso ya Kristo, furahini; ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe. (1 Petro 4:12-13)

11 Mwanangu, usidharau kuadhibiwa na BWANA, Wala usione ni taabu kurudiwa naye. 12 Kwa kuwa BWANA humrudi ampendaye, kama vile baba mwanawe ampendaye. (Mithali 3:11-12)

5 tena mmeyasahau yale maonyo, yasemayo nanyi kama kusema na wana, Mwanangu, usiyadharau marudia ya Bwana, Wala usizimie moyo ukikemewa naye; 6 Maana yeye ambaye Bwana ampenda, humrudi, Naye humpiga kila mwana amkubaliye.

7 Ni kwa ajili ya kurudiwa mwastahimili; Mungu awatendea kama wana; maana ni mwana yupi asiyerudiwa na babaye? 8 Basi kama mkiwa hamna kurudiwa, ambako ni fungu la wote, ndipo mmekuwa wana wa haramu ninyi, wala si wana wa halali. 9 Na pamoja na hayo tulikuwa na baba zetu wa mwili walioturudi, nasi tukawastahi; basi

si afadhali sana kujitia chini? 10 Maana ni hakika, hao kwa siku chache waliturudi kama walivyoona vema wenyewe; bali yeye kwa faida yetu, ili tuushiriki utakatifu wake. 11 Kila adhabu wakati wake haionekani kuwa kitu cha furaha, bali cha huzuni; lakini baadaye huwaletea wao waliozoezwa nayo matunda ya haki yenye amani. (Waebrania 12:5-11)

Mateso yanaruhusiwa ili kwamba watu warekebishwe, wafundishwe, wajenge tabia, na wawe wema kupitia mateso (Tazama pia Warumi 5:3-4, 8:17; 2 Wathesalonike 1:3-5; Yakobo 1:2-4; 2 Petro 1:5-8; Ufunuo 21:7-8). Majaribu na shida zinasaidia kujenga imani, kufundisha unyenyekevu, kutufundisha masomo, na pia yanasaidia kutuleta karibu na Mungu.

Hata kama inaonekana kutulemea sasa, Mungu anaelewa na anawezesha watu wake kustahimili mateso na majaribu (1 Wakorintho 10:13). Yesu alifundisha kwamba kila siku yatosha kwa shughuli zake (Mathayo 6:34). Na kile ambacho amepanga siku za usoni ni zaidi ya mateso ya kimwili tunayoyapitia katika maisha haya (Warumi 8:18),

Yesu pamoja na watu wa Mungu wameteseka:

1 Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo, na dhambi ile ituzungukayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu 2 tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba {Gr. stauros – mtini}, na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. 3 Maana mtafakarini sana yeye aliyestahimili mapingamizi makuu namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao, msije mkachoka, mkizimia mioyoni mwenu. (Waebrania 12:1-3, Biblia ya Jubile)

Mateso yataisha:

12 ... Ingawa nimekutesa, sitakutesa tena; 13 Na sasa nitakuvunjia nira yake, nami nitakupasulia mafungo yako. (Nahumu 1:12-13)

Wakati neno hili lilitolewa kama unabii unaohusiana na Ninawi, maandiko mengine yanathibitisha kwamba mateso yatakwishwa (Ufunuo 21:4) na nira ya Shetani

itavunjwa (Isaya 14:12-17;Ufunuo 20:1-3).

Twapaswa kujua kwamba mara nyingi mateso hayatokani na matendo yetu.Sisi,kama vile Yesu,twaweza kuteseka bila sababu:

19 Maana huu ndio wema hasa,mtu akivumilia huzuni kwa kumkumbuka Mungu,pale ateswapo isivyo haki. 20 Kwa maana ni sifa gani kustahimili,mtendapo dhambi na kupigwa makofi? Lakini kustahimili,mtendapo mema na kupata mateso huu ndio wema hasa mbele za Mungu.

21 Kwa sababu ndio mliloitiwa;maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu,akiwaachia kielelezo, mfuatae nyayo zake.

22 Yeye hakutenda dhambi,wala hila haikuonekana kinywani mwake.

23 Yeye alipotukanwa,hakurudisha matukano; alipoteswa, hakuogofya,bali alikabidhi kwake yeye ahukumuye kwa haki. (1 Petro 2:19-23)

Yesu alitupatia kielelezo kuhusu mateso (1 Petro 2:21-24). Kama vile manabii (Yakobo 5:10-11).

Twapaswa kuwaiga manabii (1 Peter 2:21-24), na Mtume Paulo pia (1 Corinthians 13:2) kama vile alivyomuiga Yesu(1 Wakorintho 11:1).

Watoto

Je! Nini inahusu watoto wale wanaoteseka?

Biblia inatuambia kuhusu watoto wanaoteseka.Kuna mtu mmoja aliyezaliwa kipofu ili " kazi za Mungu zidhihirishwe ndani yake" (Yohana 9:3).Lakini sababu nyingine ni kwamba watajenga tabia pia.

Mungu ana mpango kwetu,hata kabla hatujazaliwa:

16Macho yako yaliniona kabla sijakamilika;Chuoni mwako ziliandikwa zote pia.Siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado. (Zaburi 139:16)

Je! Na wale watoto wanaokufa ama mimba yao hutolewa au wanaouawa wangali wachanga?

Wakati jambo hilo ni misiba inayopata wanadamu,Mungu ana mpango na wao-Hajawasahau (Isaya 49:15).Wao,pamoja na wale wasioitwa na kuchaguliwa katika dahari hii,watakuwa sehemu ya

ufufuo wa pili (Ufunuo 20:5,11).Na Biblia inasema kwamba watakuwa hai tena-na kwa wakati huo kwa miaka 100 kulingana na Isaya 65:20.

Kuelekea Utimilifu

Katika Agano la Kale,Musa aliandika kwamba "kazi ya Mungu ni kamilifu" (Kumbukumbu 32:4).Katika Agano Jipya,Mtume Yakobo aliandika:

2 Ndugu zangu,hesabuni ya kuwa ni furaha tupu,mkiangukia katika majaribu mbalimbali; 3 mifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. 4 Saburi na iwe na kazi kamilifu,mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno. 5 Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima,na aombe dua kwa Mungu,awapaye wote,kwa ukarimu,wala hakemei;naye atapewa. (Yakobo 1:2-5)

Mateso yanaonekana kama sehemu ya kuelekea utimilifu.Hayo HAYAMAANISHI kwamba tuteseke kwa hiari kama wengine wanavyofanya,lakini ni kuvumilia mateso na majaribu tunayoyapata kwa subira.

Hiyo basi ni rahisi sana kuandika kuliko kukabilia nayo-na Mungu anajua hivyo (Waebrania 12:11):

8 BWANA atanitimizia mambo yangu;Ee BWANA,fadhili zako ni za milele;Usiziache kazi za mikono yako.(Zaburi 138:8)

Mungu anafanya kazi ili apate kukukamilisha!

Kumbuka kwamba Biblia inasema kwamba Yesu alijifunza kutii kutoka kwa mateso:

8 na,ingawa ni Mwana,alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata. 9 naye alipokwisha kukamilishwa,akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii, (Waebrania 5:8-9)

Wafuasi wake pia wanapaswa kujifunza hayo.

Yesu alifundisha:

48 Basi ninyi mtakuwa wakamilifu,kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu. (Mathayo 5:48)

Je! Hiyo inamaanisha Wakristo sasa ni wakamilifu?

Hapana.

Kwa Nini Mungu Alikuumba?

Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema;na hasa jamaa ya waaminio. (Wagalatia 6:9-10)


5 ... Mungu, 6 atakayemlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake; 7 wale ambao kwa saburi katika kutenda mema wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika,watapewa uzima wa milele (Warumi 2:5-7)

Mungu anataka mema kwako na ukimpenda kwa dhati na "kumtii" (Matendo 5:32; Waebrania 5:9), mambo yatakuwa mema kwetu (Warumi 8:28).

Kumbuka yafuatayo:

24 Mwanadamu hapati jema kupita kula na kunywa,na kuiburudisha roho yake kwa mema katika kazi yake.Hayo nayo naliona ya kwamba hutoka mkononi mwa Mungu. (Mhubiri 2:24)

12 Mimi najua ya kwamba hakuna jema kwao kupita kufurahi,na kufanya mema maadamu wanaishi 13 Tena ni karama ya Mungu kila mtu apate kula na kunywa,na kujiburudisha



kwa mema katika kazi yake yote. 14 Najua ya kwamba kila kazi aifanyayo Mungu itadumu milele;haiwezekani kuizidisha kitu,wala kuipunguza kitu;nayo Mungu ameifanya ili watu wamche yeye. (Mhubiri 3:12-14)

Hayo ni ukweli,hasa kwa sababu kuwa mafanikio katika kazi kunafaa kufanya vitu viwe na mafanikio .Na wadamu wanapaswa kufurahi kuwa na mafanikio

Zaidi ya hayo,mpango wa Mungu unajumuisha yale ambayo yamekutendeka . Kumbuka

mafundisho ya Agano la Kale kuhusu hayo:

11 Shauri la BWANA lasimama milele,Makusudi ya moyo wake vizazi na vizazi. 12 Heri taifa ambalo BWANA ni Mungu wao,Watu aliowachagua kuwa urithi wake. 13 Toka mbinguni BWANA huchungulia,Huwatazama wanadamu wote pia. 14 Toka mahali pake aketipo Huwaangalia wote wakao duniani 15 Yeye aiumbaye mioyo yao

Iliendelea kwenye ukurasa unaofuata 22

Mtume Yohana alifundisha kwamba Wakristo wa kweli bado watafanya dhambi na wanahitaji maungamo (1 Yohana 1:8-10).

Kwa hiyo,ina maana kwamba Wakristo wanapaswa kusema kwamba haiwezekani na kuwacha kujaribu kuwa wakamilifu?

Hapana.

Wakristo wanapaswa kushinda kwa uwezo wa Mungu (Warumi 12:21;Wafilipi 4:13;1 Yohana 4:4) majaribu na mateso katika maisha yanatusaidia kufika karibu na ukamilifu (Yakobo 1:2-4).

Mtume Paulo wakati alipokuwa kwenye mateso,alinena jambo fulani aliloambiwa na Yesu:

9 Naye akaniambia,Neema ya Mungu yakutosha;maana uwezo wangu hutimilika katika udhaifu.Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi,ili uweza wa Kristo ukae juu yangu. (Wakorintho 12:9)

Tunakamilishwa sasa kupitia kwa yale tunayoyapitia.

Wakati Wakristo watafufuka kama watoto wa Mungu ndio watakuwa wakamilifu (Waefeso 4:13;Waebrania 11:40).

Ndiyo,kuna mambo mazuri yaliyo ghalani.Kupata kujifunza mengi,basi tazama nakala itakayotolewa baada ya hii.

Iliendelea kutoka ukurasa uliopita...

Kitabu hiki ni cha bure,kwa mtandao wetu wa ccog.org,kinaitwa Siri ya Mpango wa Mungu:

Je! Kusudi lako ni gani?

WEWE hufanani na ye yote yule.Biblia inafundisha kwamba “viungo vyote havitendi kazi moja...na viungo kila mmoja kwa wenzake...Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka” (Warumi 12:4-5,1 Wakorintho 12:18).

Kwa hivyo,uko tofauti.Hatima yako ni ya kipekee na ya muhimu.Maisha yako yana maana.

Maana ya maisha yako ya kibiblia ni gani?

Wewe ni nani?

WEWE ni mtu ambaye anaweza kutoa upendo kwa njia ya kipekee.

Na hilo ni jambo utakalofanya milele.

Kati ya karne iliyopita,Kanisa la Mungu (la Kisabato) lilichapisha yafuatayo:

Wakristo hawaishi maisha ya leo peke yake ;anatazamia maisha ya kesho. (Imani ya Kanisa. Mtetezi wa Biblia na Mpiga mbiu wa Ufalme wa Mungu. Oktoba 3, 1949, uk. 7)

Lakini sio kwamba Mkristo anatarajia kesho iliyo mema pekee.Mkristo pia anajenga tabia sasa kupitia majaribio,nafasi na hukumu katika maisha (Warumi 5:1-4) ambayo yanasaidia Mkristo kupata kuchangia mwenyewe kwa “kesho iliyo bora.”

Hatimaye Mungu ana mpango wa kipekee na wewe.

Mungu alikuumba ili utoe upendo kwa njia yako mwenyewe(1 Wakorintho 12:20-13:10).

Lakini kwa jinsi gani?

Hasa kwa kuishi kwa imani na kumtii Mungu katika maisha haya.

Kwa kutii,kufanya uamuzi wa kibiblia,kuwa na imani,kuonyesha upendo,na kufanya bidii hadi mwisho,Wakristo watajenga tabia na pia kuufanya uzima wa milele kuwa mzuri kwao na kwa watu wengine.

Kwa habari za imani,twajua ya kwamba kuwepo kwa Mungu ni ukweli (Warumi 1:20; tazama pia kitabu chetu ambacho kinapatikana kwenye tovuti ya ccog.org,yaani Je! Kuwepo kwa Mungu ni kimantiki?),haihitaji imani kusadiki kwamba Mungu yupo.Hata mapepo waamini na kutetemeka (Yakobo 2:19).Hata hivyo haiitaji imani kusadiki,kuamini na kumtii Mungu.Hiyo ni sehemu ya “siri ya imani” (1 Timotheo 3:9;Zaidi kuhusu Imani pia tazama kijitabu chetu cha mtandao yaani ccog.org,yaani Imani kwa wale walioitwa na kuchaguliwa).

Mungu anawapa Roho Mtakatifu kwa wale wamtio (Matendo 5:32).Ukweli ni kwamba Roho Mtakatifu ndiyo inafanya mtu kuwa Mkristo wa kweli (Warumi 8:9-11).

Wakristo wenyewe baadaye watabadilishwa na kukamilishwa kwenye ufufuo wakwanza (1Wakorintho 15:50-54;Ufunuo 20:5-6 ili wapate kusaidia kutoa upendo na kuweka uzima wa milele uwe bora.Ufufuo huu unaingiana na baragumu ya saba na ya mwisho (1 Wakorintho 15:52),ambapo ndiyo sehemu ya siri ya Mungu itakapokwisha (Ufunuo 10:7).

Mtume Paulo anarejelea mabadiliko yenyewe kama “siri” (1 Wakorintho 15:51).

Wale ambao sio Wakristo watakuwa na nafasi ya mabadiliko katika ufufuo utakaofanyika baadaye (tazama kitabu chetu katika mtandao wa ccog.org,Universal OFFER of Salvation,Apokatastasis:Can God save the lost in age to come? Hundreds of scriptures reveal God’s plan of salvation).

Tenda Wema

Mungu ni mwema (Marko 10:18; Zaburi 143:10) na anafanya kilicho chema (Mwanzo 18:25).

Mungu pia anataka tufanye vyema kama inavyompendeza (Zaburi 34:14; Waebrania 13:16).

19 Mkuu wa mashauri,mweza katika kutenda;ambaye macho yake yamefumbuka juu ya njia zote za wanadamu,kumpa kila mtu kwa kadiri ya njia zake,na kwa kadiri ya matendo yake. (Yeremia 32:19)

9 Tena tusichoke katika kutenda mema;maana tutavuna kwa wakati wake,tusipozimia roho. 10

wote Huzifikiri kazi zao zote. (Zaburi 33:11-15)

1 Na kwa ajili ya hayo yote, nikatia moyo wangu katika kuyatafuta-tafuta haya; ya kuwa wenye haki, na wenye hekima, pamoja na matendo yao yote, wamo mkononi mwa Mungu; (Mhubiri 9:1a)

9 Moyo wa mtu huifikiri njia yake; Bali BWANA huziongoza hatua zake. (Mhubiri 16:9)

24 Mwenendo wa mtu watoka kwa BWANA; Basi, awezaje mtu kuelewa na njia yake? (Mhubiri 20:24)

73 Mikono yako ilinifanya ikanitengeneza, (Zaburi 119:73)

17 ... Mungu atawahukumu wenye haki na wasio haki; kwa kuwa kuna wakati huko kwa kila kusudi na kwa kila kazi. (Mhubiri 3:17)

Kumbuka sasa, mafungu haya katika Agano Jipya:

11 lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye. ... 27 Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo. (1 Wakorintho 12:11, 27, AFV)

7 Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna.

8 Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele. (Wagalatia 6:7-8)

10 Maana Mungu si dhalimu hata aisahau kazi yenu, na pendo lile mlilolidhihirisha kwa jina lake ... (Waebrania 6:10)

Mungu ana mpango kwa WOTE! Na hiyo ni PAMOJA NA WEWE BINAFSI hata kama umeitwa kwa wakati huu au bado. Na anakumbuka KAZI YAKO YOTE.

Chochote umepitia, shida zote umekumbana nazo, chochote umefanikisha n.k, kinakutayarisha kufanya uzima wa milele uwe bora (isipokuwa utakataa baadaye kukubali Ufalme wa Mungu). Chochote umepitia kinakutayarisha kwa wito na kazi ya Mungu amekupangia! Utakuwa unatoa kwa njia ya kipekee na kusaidia kuboresha uzima wa milele!

Biblia imetaja kwamba kama vile mwili una sehemu kama mikono na macho na sehemu ya kunusa, kusikia na vitu vingine (1 Wakorintho 12:12-26), pia tunao sehemu ya kipekee katika mpango wa milele ambao Mungu amepanga. Ndiyo, jukumu lako laweza kuwa tofauti na mabilioni ya watu-usidhani kwamba Mungu hana mpango halisi na WEWE.

Zaidi ya hayo, una wajibu kwa kile unachokifanya (Warumi 14:12). Mungu atahukumu kulingana na yale unayoyatenda (Mhubiri 12:14; Ufunuo 20:12) na pia yale ambayo umeyakataa kufanya (Mathayo 25:24-30). Kadiri unavyozidi kufanya yale unapaswa kufanya, ndiposa utafanya uzima wako wa milele uwe bora sana kwako na wengine. Mungu ni mhukumu mwenye haki (2 Timotheo 4:8).

Biblia inasema kwamba tutatuzwa kulingana na kazi yetu (Mathayo 16:27; Warumi 2:6; Mithali 24:12; Yeremia 17:10; Ufunuo 22:12)! Na tutaweza kusaidia watu wengi kwa sababu ya hiyo (Luka 19:15-19). Biblia inasema kwamba baada ya kifo, kazi yetu inatufuata (Ufunuo 14:13)-ambayo ina maana kwamba kile ambacho tumejifunza na kuendeleza tukiwa katika maisha haya yatasaidia kwa kutoa na kufanya kazi kwa maisha ya uzima wa milele mzima.

Chochote ambacho Mungu amefanya amekuwa na sababu ya kufanya hivyo (Ezekieli 14:23). Pamoja na muda tunaochukua katika maisha haya ambayo pia ni siri tusiyoweza kujua (Mhubiri 9:12).

"Mwamini Mungu" (Marko 11:22) kwa sababu ana sababu nzuri sana kwa kila jambo analolifanya-hata kama halionekani zuri kwetu sisi (Waebrania 12:11; Warumi 8:28)

Wengi wamemhukumu Mungu kimakosa kulingana na fikra zao, japo Biblia pia inafundisha yafuatayo:

5 Basi nanyi msihukumu neno kabla ya wakati wake, hata ajapo Bwana; ambaye atayamulikisha yaliyositirika ya giza, na kuyadhihirisha mashauri ya mioyo; ndipo kila mtu atakapoipata sifa yake kwa Mungu. (1 Wakorintho 4:5)

Mambo mengine yamesitirika. Na pia sisi hatujui kila kitu kuhusu mtu ye yote.

Watu wote hawalingani. Mungu ana mpango kwa kila mmoja (1 Wakorintho 12:4-12).

Mungu anafanya kazi na wote ili kwamba kila mmoja wetu awe na sehemu katika uzima wa milele! Kama maandiko yanavyofundisha:

17 Na kazi ya haki itakuwa Amani,na mazao ya haki yatakuwa ni utulivu na matumaini daima. (Isaya 32:17)

11 Utanijulisha njia ya uzima;Mbele za uso wako ziko furaha tele;Na katika mkono wako wa kuume Mna mema ya milele. (Zaburi 16:11)

Amani na radhi milele.Uzima wa milele ulio bora!

Ni nini UNATAKIKANA UFANYE?

11 Njoni enyi wana, mnisikilize, Nami nitawafundisha kumcha BWANA. 12 Ni nani mtu yule apendezwaye na uzima, Apendaye siku nyingi apate kuona mema? 13 Uuzie ulimi wako na mabaya,Na midomo yako na kusema hila. 14 Uache mabaya ukatende mema, Utafute Amani ukaifuatie. (Zaburi 34:11-14)

3 Umtumaini BWANA ukatende mema,Ukae katika nchi,upendezwe na uaminifu. 4 Nawe utajifurahisha kwa BWANA,Naye atakupa haja za moyo wako. (Zaburi 37:3-4)

TENDA WEMA! MWAMINI MUNGU!.

Haya yote yanamaanisha nini?

Ina maana kwamba Mungu aliumba kile alichokiumba ili uumbaji wake upate kufanya vyema.

Ama kwa hakika,Mungu aliumba kila kitu ili kwamba uzima wa milele uwe bora! Jambo hilo si ni la ajabu!

3 ... Ni makuu,na ya ajabu,matendo yako,Ee Bwana Mungu Mwenyezi! (Ufunuo 15:3)

19 Jinsi zilivyo nyingi fadhili zako Ulizowawekea wakuchao;Ulizowatendea wakukimbiliao Mbele ya wanadamu! (Zaburi 31:19)

Wema wa Mungu ni mkuu kwa sababu ya kile ambacho ametuandalia.

Katika Waebrania 11:4-12,kuanzia Abeli,tumejifunza kuhusu watu wengi walioitwa na Mungu katika Agano la Kale:

13 Hawa wote wakafa katika imani,wakiwa

hawajazipokea zile ahadi,bali wakazona tokea mbali na kuzishangilia,na kukiri kwamba walikuwa wageni,na wasafiri juu ya nchi. 14 Maana hao wasemao maneno kama hayo waonyesha wazi kwamba wanatafuta nchi yao wenyewe. 15 Na kama wanalikumbuka nchi ile waliyotoka,wanalipata nafasi ya kurejea . 16 Lakini sasa waitamani nchi iliyo bora,yaani ya mbinguni.Kwa hiyo Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao;maana amewatengenezea mji. (Waebrania 11:13-16)

Kwa hivyo tangia wakati wa Abeli,watu wamekuwa na imani kwamba Mungu ana mpango wa kitu bora,na kuwa Mungu ni Mungu wa wale wanaolewa mpango huo. "Mji" ni Yerusalemu ambao utashuka duniani kutoka mbinguni (Ufunuo 21:2).

Mpango ni kwamba mambo yawe mema.

Kumbuka yafuatayo kutoka Agano Jipya:

17 Basi yeye ajuaye kutenda mema,wala hayatendi,kwake huyo ni dhambi.. (Yakobo 4:17)

Je! Jambo hilo lina maana kwamba Wakristo wanapswa kutenda mema?

Kutenda mema ni kufanya vitu viwe bora.

Jinsi Kanisa la Awali Lilikuwa Likifanya Mema na Kuabudu

Waandishi wa Kanisa la awali walikuwa na uelewa fulani na wakadokezea kuhusu kusudi ya siri ya mpango wa Mungu.

Katika karne ya pili (B.K.) Polycarp wa Smirna ,aliyewekewa mikono na mtume mmoja au wengine,aliandika:

Tufanye jitihada katika kutafuta kile kilicho chema (Barua ya Polycarp kwa Wafilipi,mlango wa 6)

Yeye (Yesu) alifundisha... matunda ya ujira wa milele.(Polycarp,Fragments Kutoka kwa Victor wa Capua,sehemu ya 4)

Tena,Melito wa Sarde,ambaye alikuwa mwandamizi wa Polycarp,aliandika:

Amempa yeye akili iliyojawa na uhuru;ameweka mbele yake vifaa kwa idadi kubwa,ili kwamba

kwa upande wangu naweza kutofautisha asili ya kila kitu na kuchagua kile kilicho bora; (Melito. A Discourse Which Was in the Presence of Antoninus Caesar. In Ante-Nicene Fathers by Roberts and Donaldson, Volume 8, 1885. Hendrickson Publishers, Peabody (MA), printing 1999, p.755).

Kujifunza kufanya mema kunajenga tabia..Tukichagua kufanya mema tunasaidia kufanya vitu kuwa vizuri. Melito alielewa kwamba Mungu aliwapa uhuru wa kuchagua na tunapaswa kuchagua mema. Hata kama Adamu na Hawa walichagua kupotoka, ambako kulisababisha utumwa (Warumi 6:16-17), Melito alieleza yafuatayo:

Lakini mwanadamu, ambaye kiasili ana uwezo wa kupokea mema na mabaya kama vile udongo wa nchi unaweza kuzipokea mbegu kwa pande zote, alikaribisha mshauri mlafi na mwenye uhasama, na kwa kuuza ule mti alihalifu amri, na kukosa kumtii Mungu. (Melito. The Homily On the Passover, line 48)

Melito pia alielewa kwamba Yesu alikuwa sehemu ya mpango wa kutuokoa kutoka kwa utumwa wa dhambi:

Siri ya Pasaka ni mpya na ya kale, ya milele na ya muda, kinachoharibika na kisichoharibika, kinachokufa na kisichokufa... Kwa hivyo ukweli ni kwamba siri ya Bwana ni ya kale na mpya... Kwa kupitia sauti ya unabii ndio siri ya Bwana ulitangazwa. ...Yeye ndiye alituochoa kutoka kwa utumwa na kutuleta kwa uhuru, kutoka gizani hadi nuruni, toka mauti hadi uzimani, toka dhuluma hadi ufalme wa milele, na aliyetufanya kuwa ukuhani mpya, na watu wa kipekee milele. (Melito. The Homily on the Passover by Melito, lines 2, 58, 61, 68).

Ndiyo, Ufalme ni wa milele. Na ni kupitia siri ya unabii- unabii ambao haukueleweka vile ungeeleweka na viongozi wa dini wa wakati wa Yesu-Yesu alitangazwa kabla hajaja bado (kwa unabii mia na zaidi, tazama kitabu chetu kwa mtandao wa www.ccog.org kinachoandikwa: Proof Jesus is Messiah). Siri nyingine inayohusiana na Pasaka ni kwamba Yesu alivunja mkate na akawapa wanafunzi kipande cha kipekee (Luka 24:30), ambayo kwa wale ambao wanatunza Pasaka kamili ya Wakristo leo (ambayo wakati

mwingine huitwa Ekaristi), wanasaidia kuonyesha kwamba Mungu ana kitu cha ajabu kwa kila mmoja na pia kwa wale wengine wa kipekee.

Irenias wa Lyoni alidai kwamba alifundishwa na Polycarp wa Smirna. Irenias aliandika kwamba Wakristo wana "tumaini wa ufufuo na kuingia katika uzima wa milele" (Irenaeus. Against Heresies, Book IV, Chapter 18, para 5). Ukweli ni kwamba Wakristo watakaofufuka wataishi milele.

Zaburi inafundisha:

20 Wewe, uliyetuonyesha mateso mengi, mabaya, utatuhuisha tena. Utatupandisha juu tena Tokea pande za nchi. 21 Laiti ungeniongezea ukuu! Urejee tena na kunifariji moyo. (Zaburi 71:20-21)

Baada ya ufufuo (pia unaitwa kuhuisha tena) Mungu ataongeza ukuu wa watumishi wake.

Atafanya kwa jinsi gani?

Mungu alitaja kwamba "Ndinyi miungu" (Yohana 10:34) na sehemu ya Zaburi 82:6 ambayo inafundisha kuhusu kuinuliwa kwa wale watakoishi kwa njia ya Mungu.

Irenias pia alifundisha:

... Hakuna ye yote aitwaye Mungu na maandiko bali tu ni Baba ya wote, na Mwana, na wale wanaofanywa wana (Irenaeus. Adversus haereses, Book IV, Preface, Verse 4) "Nilisema kwamba ninyi ni wana wa Aliye Juu, miungu; lakini mtakufa kama wanadamu." Anaongea bila maneno haya waziwazi kwa wale ambao hawajapokea zawadi ya kufanywa wana, lakini wanadharau kufanywa upya kwa Neno la Mungu, ambaye alikuwa mwili kwao. Na ni kwa sababu ya hiyo ndiyo Neno la Mungu likafanywa mtu, na huyo aliyekuwa Mwana wa Mungu akawa Mwana wa binadamu, huyo binadamu baada ya kuchukuliwa kwa Neno, na kufanywa wana, wanaweza kuwa wana wa Mungu. Kwa sababu hakuna njia nyingine ambayo tungefikia hali ya kutoharibika na kutokufa. (Irenaeus, Adversus haereses, Book III, Chapter 19, Verse 1).

Mtume Yohana aliandika:

2 Wapenzi,sasa tu wana wa Mungu,wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa;lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa,tutabadilika kuwa naye;kwa maana tutamwona kama alivyo. (1 Yohana 3:2,Utafsiri wa Biblia ya Darby)

Kwa vile Yesu hakuwa amerudi,Wakristo hawajabadilika kuwa kama yeye-lakini kubadilika kuwa kama yeye ni sehemu ya mpango (1 Wakorintho 15:50-53).Bado kuna siri kuhusu vile tutakavyokuwa (1 Wakorintho 13:12),lakini mpango wa Mungu unahusu kufanywa wana (Warumi 8:29;Matendo 17:29;Mathayo 5:48;Waefeso 3:14-19;Malaki 2:15).

Katika karne ya pili,Ignasia wa Antiokia aliandika:

Siyotabiayangukujifanyakama anayemfurahisha mtu,lakini kumpendeza Mungu,na hata ninyi mpendeze Mungu.Kwa sababu sitakuwa na fursa tena ya kumfikia Mungu-ambaye anapewa utukufu kwa kazi njema...Ni vizuri kuepukana na ulimwengu na kumrudia Mungu,ili nifufuke kwa yeye...Niwache niteseke kwa kuliwa kama chakula cha wanyama pori,kupitia kwa mbinu ya mtu ye yote lakini nitakuwa nimemfikia Mungu... Natamani kikombe cha Mungu,yaani damu yake ambayo ni upendo usioharibika na uzima wa milele.(Ignasia.Barua kwa Warumi,Sura 2,4).

Yeye ndiye mlango wa Baba ambaye katika yeye Ibrahimu na Isaka na Yakobo na manabii,na mitume na Kanisa wanaingia.Hivi vyote ni vifaa vya kufikia umoja wa Mungu.(Ignasia.Barua kwa Warumi,Sura 9)

Kwa hivyo,Ignasia alifundisha kwamba lengo la watu wa Mungu ni kufanywa wana na kufanya kazi njema iliyo ya milele.

Baadaye katika karne ya pili,Theofila wa Antiokia aliandika:

Kwa wale ambao kwa subira wanazidi kufanya vyema wakitafuta kuishi milele,atawapa uzima wa milele,furaha,amani,pumziko na vitu vizuri ambavyo jicho halijaona,na sikio kusikia na halijaingia katika moyo wa mwanadamu. (Theophilus.To Autolycus,Book I,Chapter 14). Pia baada ya mwanadamu kuumbwa katika ulimwengu huu,imeandikwa kama fumbo katika Mwanzo,kana kwamba aliwekwa mara

mbili ndani ya Paradiso;ili kwamba unabii wa kwanza upate kutimika wakati aliwekwa hapo na wa pili utatimika wakati wa ufufuo wa wafu na hukumu.Kwa sababu kama chombo,wakati anaundwa anakuwa na kasoro,basi analainishwa na kutengenezwa tena,ili kwamba awe mpya na mzima;na inafanyika pia mtu akifa.Kwa njia nyingine anavunjwa ili afufuke akiwa mzima;yaani bila mawaa,na mwenye haki,na asiyeweza kufa tena...

Kwa sababu ikiwa angemuumba na mwili usiokufa kuanzia mwanzo,angemuumba kama Mungu...ili kwamba ikiwa atatazama mambo ya kutokufa,kutunza amri za Mungu,anapaswa kupokea ujira wa kutokufa kutoka kwa Mungu,na anapaswa kuwa kama Mungu... Kwa sababu Mungu ametupatia sheria na amri takatifu;na ye yote ambaye atazitunza ataokoka,na kufikia ufufuo,na kuweza kurithi kutoharibika (Theophilus of Antioch.To Autolycus,Book 2,Chapters 26,p.105).

Ye yote atakayetenda kwa haki ataepa adhabu ya milele,na atastahili uzima wa milele kutoka kwa Mungu.(Theophilus.To Autolycus,Book II,Chapter 34)

Lakini wale wanaomwabudu Mungu wa milele,wataurithi uzima wa milele (Theophilus. To Autolycus, Book II, Chapter 36)

Na tumejifunza sheria takatifu;lakini tuna mpaji wa sheria ambaye yeye ni Mungu,ambaye anatumfundisha tutende haki na kuwa wacha Mungu na kutenda mema.(Theophilus. To Autolycus, Book III, Chapter 9)

Kwa hivyo Theofila alifundisha kufanywa wana na kutenda mema kwa wale Wakristo wa kweli.

Katika karne ya tatu,mtakatifu wa Katoliki na pia Askofu Hipolita wa Rumi aliandika:

Baba aishiye milele alituma Mwana aishiye milele na Neno katika ulimwengu,ambaye alikuja kama mwanadamu ili kwamba apate kusafishwa na maji na Roho;na kwa kutuzaa tena kwa roho na mwili zisizoharibika,alitupulizia pumzi (roho) ya uhai na kutuvumilia kwa mlolongo wa kile kinachoharibika.Ikiwa kama mwanadamu atakuwa kiumbe kisichokufa,basi atakuwa kama Mungu.Na ikiwa atafanyika Mungu kwa maji na

Roho Mtakatifu baada ya kuhuisha kwa safu basi atapatikana pia kuwa mrithi sawasawa na Kristo baada ya ufufuo kutoka kwa wafu (Hippolytus. The Discourse on the Holy Theophany, Chapter 8). Kwa sababu kwa kuendelea katika maadili, na kufikia mambo mazuri, “nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachumulia yaliyo mbele,” (Wafilipi 3:13, KJV) kulingana na neno la mbarikiwa Paulo, twapanda juu kwa uzuri ulio wa juu. Namaanisha uzuri wa kiroho ili kwamba hata kwetu sisi isemekane badaye, “Mfalme aliutamani uzuri wenu.” (Hippolytus. Fragments from the Scriptural Commentaries of Hippolytus)

Basi Hipolitas alifundisha kufanywa wana na kwamba Wakristo watafikia mambo mema kwa kuendelea katika maadili. Katika karne ya 4, mtakatifu wa Wagiriki-Rumi na Askofu Ambrose wa Milani alifundisha:

Na Bikira akazaa, na Neno likawa mwanadamu na huyo akawa Mungu (Ambrose of Milan. Concerning Virginity Book I, Chapter 11).

Katika karne ya 4, mtakatifu wa Othodoksi na Askofu John Chrysostom aliandika:

... mtu anaweza kuwa Mungu, na kuwa mwana wa Mungu. Kwa sababu twasoma, “Nimesema ninyi miungu, na nyinyi nyote ni wana wa Aliye Juu” (John Chrysostom. Homily 32 on the Acts of the Apostles).

Kufanywa wana umeeleweka kwamba lilikuwa lengo kwa wanadamu tangia wakati wa Yesu.

Jaribu Kufanya Mema

Sulemani aliandika kwamba watu wanapaswa kutafakari kazi ya Mungu (Mhubiri 7:13). Watu wengi hawaelewi kazi ya Mungu ama hawatafakari vyema kazi hiyo-lakini wanapaswa kutafakari (Mathayo 6:33). Kuna kazi ya kufanywa kutekeleza kazi ya Mungu (Mathayo 24:14, 28:19-20; Warumi 9:28; 2 Wakorintho 9:6-8; Ufunuo 3:7-10). Na hiyo itakuwa vyema kufanywa (2 Wakorintho 9:6-14; Ufunuo 3:7-13).

Biblia mara nyingi inasema “fanya mema.” Twatenda mema kwa kusaidia wengine. Twatenda mema kwa kumpenda Mungu na majirani (Mathayo 22:37-39)—na watu wengine.

Wakristo wanapaswa kusaidia kwa kazi ya Mungu ili ifikie wengine (Mathayo 24:14, 28:19-20; Warumi 10:15, 15:26-27).

Kusudi la kazi ni kuweka vitu sawa:

5 Mawazo ya wenye bidii huulekea utajiri tu, (Mithali 21:5a)

23 Katika kila kazi mna faida, (Mithali 14:23)

23 Katika kila ajira kuna manufaa (Mithali 14:23, Tafsiri ya Kawaida la Young)

Kufanya kazi kunafaa kuleta faida (manufaa) kwa wote.

Mtume Paulo aliandika:

12 Basi, wapendwa wangu, kama vile mlivyotii siku zote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi sana nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka 13 Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu. (Wafilipi 2:12-13)

Twapasa kufanya kazi kwa kufurahisha Mungu-ambako kutaongeza upendo na kufanya uzima wa milele bora:

15 Wewe ungeita, nami ningekujibu; Ungekuwa na tamaa ya kazi ya mikono yako.. (Ayubu 14:15)

WEWE pia ni kazi ya mikono ya Mungu! Ana mpango na wewe na huo ni pamoja na kufanya kazi ili usaidie kufanya uzima wa milele uwe bora.

Mwandishi Maria Popova alifanya uchunguzi ufuatao:

Siri ambayo inafanya nafsi yako na ya utotoni mwako kuwa sawa licha ya mabadiliko hasa ni swala la ajabu ya filozofia. (Popova M. Grace Paley on the Art of Growing Older. Brain Pickings, September 3, 2015)

Kile ambacho ni siri kwa watu wengi siyo siri kwa Mungu. Mungu anafanya kazi na sisi sote ili atusaidie tuwe bora iwezekanavyo.

Kumbuka kwamba sababu ya kuvumbua vitu ni kufanya vitu kuwa bora.

Sababu ya Mungu “kuvumbua” wanadamu ni kufanya

uzima wa milele kuwa bora

Paulo na Barnaba walisema:

18 Asema Bwana,ajulishaye hayo tangu milele..
(Matendo 15:18)

Mungu aliwaumba watu na kuwaweka hapa duniani
kama sehemu ya mpango wake wa kazi njema:

8 Kwa maana mmeokolewa kwa neema,kwa
njia ya imani;ambayo hiyo haikutokana na nafsi
zenu,ni kipawa cha Mungu;

9 wala si kwa matendo,mtu awaye yote asije
akajisifu. 10 Maana tu kazi yake,tuliumbwa katika
Kristo Yesu,tutende matendo mema,ambayo
tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende
nayo. (Waefeso 2:8-10)

Watu wote?

Wote watakaokubali mpango wa Mungu watafanya
uzima wa milele bora.Na hao watakuwa wote
walioishi isipokuwa wale waovu watakaokataa wito.
(ukitaka kupata mafundisho haya zaidi, tazama kitabu
chetu kwa mtandao wa tovuti: Universal OFFER of
Salvation, Apokatastasis: Can God save the lost in
an age to come? Hundreds of scriptures reveal God's
plan of salvation).

Yesu alieleza kwamba kuna makao kwa kila mmoja
wetu:

1 Msifadhaike mioyoni mwenu;mwamini
Mungu,niaminini na mimi pia. 2 Nyumbani
mwa Baba yangu mna makao mengi;kama
sivyo,ningaliwaambia;maana naenda
kuwaandalia mahali 3 Basi mimi nikienda na
kuwaandalia mahali,nitakuja tena niwakaribishe
kwangu;ili nilipo mimi,nanyi mwepo . (Yohana
14:1-3, BSB)

Kuwaandalia mahali ina maana kwamba Yesu anaahidi
mahali ambapo patakuwa pema kwako.Mahali
ambapo patasaidia kutumia uwezo wako.Usidhani
kwamba wewe huwezi kuwa na furaha na kuchangia
katika Ufalme wa Mungu.Mungu ni mwaminifu wa
kumaliza kazi aliyoianza kwako (Wafilipi 1:6).

Mpango wa Mungu kwa wanadamu utadumu milele:

14 Najua ya kwamba kila kazi aifanyayo Mungu

itadumu milele;haiwezekani kuzidisha kitu wala
kuipunguza kitu.. (Mhubiri 3:14)

Biblia inaonyesha kwamba Yesu alikuja mwenyewe
kufanya vitu kuwa bora:

6 ... kwa kadiri alivyo mjumbe wa agano lilio
bora,lililoamriwa juu ya ahadi zilizo bora.
(Waebrania 8:6)

Wakristo wana tumaini kwa mambo mema-na jambo
hilo lafaa litufaraji:

19 ... kuliingizwa matumaini yaliyo mazuri
zaidi,ambayo kwa hayo twamkaribia Mungu.
(Waebrania 7:19)

13 Lakini,ndugu,hatutaki msijue habari
zao waliolala mauti,msije mkahuzunike
kama na wengine wasio na matumaini. 14
Maana,ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa
akafufuka,vivyo hivyo na hao waliolala katika
Yesu,Mungu atawaleta pamoja naye.

15 Kwa kuwa twaambieni haya kwa neno la
Bwana,kwamba sisi tulio hai,tutakaosalia
hata wakati wa kuja kwake Bwana,hakika
hatutawatangulia wao waliokwisha kulala
mauti. 16 Kwa sababu Bwana mwenyewe
atahuka kutoka mbinguni na mwaliko,na sauti
ya malaika mkuu,na parapanda ya Mungu;nao
waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza.
17 Kisha sisi tulio hai,tuliosalia,tutanyakuliwa
pamoja nao katika mawingu,ili tumlaki Bwana
hewani;na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana
milele. 18 Basi farijianeni kwa maneno hayo. (1
Wathesalonike 4:13-18)

34 ... mkijua kwamba nafsini mwenu mna mali
iliyo njema zaidi,idumuyo. (Waebrania 10:34,
BLB)

Mungu aliumba kila kitu ili kwamba uzima wa milele
uwe bora.Uzima huo utakuwa mwema milele (Yere
mia 32:38-41).

Kufanya vitu viwe bora kunaridhisha Mungu,ambako
pia ni jambo jema.Na kwa hakika Mungu anaridhika
(Waebrania 11:5, 13:16; 1 Petro 2:19-20, NLT)--Jambo
hilo si ni jema kwa Mungu?

Mungu aliumba kile alichokiumba ili kwamba uzima

wa milele uwe bora.

Hiyo ndiyo maana aliumba mbingu na nchi na hiyo ndiyo maana aliumba wanaume ana wanawake.

Mpango wa Mungu ni pamoja na wale ambao wataitikia wito wake katika kipindi hiki (tazama pia: Is God Calling You?) na mengine katika kipindi kijacho (Tazama pia kitabu chetu cha mtandao: Universal OFFER of Salvation. Apokatastasis: Can God save the lost in an age to come? Hundreds of scriptures reveal God's plan of salvation).

Wakristo wanapaswa kuelewa kwamba jukumu lao la kipekee ni kufanya uzima wa milele kuwa bora.

Lakini hiyo LAZIMA ifanywe kwa njia ya Mungu.

12 Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, Lakini mwisho wake ni njiaza mauti. (Mithali 14:12; 16:25)

Kuna watu ambao wanadhani kwamba wanafanya ulimwengu kuwa bora kwa njia nyingi. Na kama inaingiliana na njia za Mungu, basi wanafanya vyema.

Kuna wengine ambao wanadhani kwamba wanafanya ulimwengu kuwa mema wakati wanafanya migomo, wakipinga utoaji wa mimba na aina nyingi ya ukosefu wa maadili unaokemewa na Biblia.

Ni watu ambao wanadhani kwamba wanafanya ulimwengu kuwa bora wakati wanaendeleza ibada ya pagani huku wakiona ni nzuri.

Cha kuhuzunisha ni kwamba watu wengi wanajishawishi na kuamini mitazamo ya wengine, mapokeo ya awali, tamaa zao, na kutumainia mioyo yao kuliko kuweka tumaini kwa Biblia. Hata hivyo maandiko yanaonya:

9 "Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua? 10 Mimi, BWANA, nauchunguza moyo, navijaribu viuno hata kumpa kila mtu kiasi cha njia zake, kiasi cha matunda ya matendo yake. (Yeremia 17:9-10)

Je! Una moyo unaotaka kufanya vitu kwa njia ya Mungu?

Hakika? Kweli?

Natumai kwamba una moyo huo.

Wakati Mungu anataka watu watende mema, wale walio na mioyo ya udanganyifu hawafanyi hivyo:

20 Mtu mwenye moyo wa ukaidi hatapata mema; Na mwenye ulimi wa upotofu huanguka katika misiba. (Mithali 17:20)

Hata kama mambo yanaonekana magumu kwa njia ya kawaida, mtumainie Mungu:

9 Mcheni BWANA, enyi watakatifu wake, Yaani wamchao hawahitaji kitu. 10 Wana-simba hutindikwa, huona njaa; bali wamtafuta BWANA hawahitaji kitu chochote kilicho chema. (Zaburi 34:9-10)

31 Msisumbuke, basi mkisema, Tule nini? Au Tunywe nini? Au Tuvae nini? 32 Kwa maana hayo yote mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. 33 Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa. 34 Basi msisumbukie ya kesho; kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Yatosha kwa siku maovu yake. (Mathayo 6:31-34)

Zidi kutumia uwezekano wako kwa kujisaidia na pia kuwasaidia wengine, mtumaini Mungu na awe mshauri wako:

5 Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, Wala usitegemee akili zako mwenyewe 6 Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako. 7 Usiwe mwenye hekima machoni pako; Mche BWANA ukajiepushe na uovu. 8 Itakuwa afya mwilini pako, Na mafuta mifupani mwako. (Mithali 3:5-8)

Usiwe mwenye hekima machoni pako kiasi cha kwamba hautatumaini Mungu.

Utakuwa heri ukimtumaini Mungu.

Fanya kazi na kusaidia kazi ya Mungu ifikie wengine.

Ndiyo, Mungu ana mpango na WEWE!

Miujiza ya Yesu-Sehemu ya 2: Mwenye Ukoma Aponywa

Na S. Perry, Mfano na C. Parr

Yesu alikuwa amemaliza kufundisha watu kuhusu Ufalme wa Mungu,watu wengi walikuwa wanamfuata aendako.

Mbele yake alisimama mtu mmoja mwenye ugonjwa wa shingo. Alikuwa amefunikwa na vigaga na vidonda. Alikuwa kwa Yesu na kujilaza mbele yake Akipiga magoti na kumwinamia kama mfalme.



Mtu huyu alijua kwamba Yesu anaweza kumponya. Basi akauliza, “Bwana,waweza kunitakasa.”

Yesu akanyosha mkono,akamgusa,akisema, “Nataka;takasika.” Na mara ukoma wake ukatakasika!

Yesu akamwambia aende ajionyeshe kwa kuhani na apeleke sadaka ya Mungu kwa kuhani.Hiyo ingemfanya kuhani amwangelie na kusema, “Kwani huyu mtu hana ugonjwa wa ukoma na yuaweza kukutana na watu wengine.”

Hangeweza kujificha kwa watu tena.Alishukuru sana kwa yale Yesu alimfanyia

KUTAFUTA NENO – Piga mistari kila nukta x,y,na Z ili utafute maneno kutoka kwa hadithi ulioisoma

x	s	i	z	c	Y	x	k	y
d	i	x	s	z	E	a	s	e
z	b	o	z	w	X	i	n	g
x	y	k	i	x	Z	n	z	g
c	y	l	z	e	A	x	n	z
t	o	y	u	c	Z	h	e	d
y	p	x	r	i	E	z	s	t

Mathayo Mlango wa 8 Mistari ya 1-4

1 Naye aliposhuka mlimani, makutano mengi walimfuata. 2 Na tazama,akaja mwenye ukoma akamsujudia, akisema, Bwana, ukitaka, waweza

kunitakasa. 3 Yesu akanyosha mkono, akamgusa, akisema Nataka, takasika. Na mara ukoma wake ukatakasika.

4 Yesu akamwambia, Angalia, usimwambie mtu;ila enenda zako, ukajionyeshe kwa kuhani, ukaitoe sadaka kama alivyoamuru Musa, iwe ushuhuda kwao.

Kujifunza zaidi

Mwujiza umelezwa kwa mistari michache lakini una maana Zaidi ya uponyaji pekee.

Kumbuka kwamba huyu mtu hakuwa kwa umati ambao walikuwa mlimani,lakini anajua nguvu aliyo nayo Yesu.Hakuwa na umati ule kwa sababu ya ukoma. Watu walikatazwa kuja karibu naye ili wasiambukizwe na ugonjwa huo.Ukoma ulikuwa ugonjwa mbaya sana,lakini matumizi ya neno ukoma waweza kumaanisha aina nyingi na magonjwa ya shingo. Kulingana na sheria,mtu aliye na ugonjwa wa ukoma hangeingia hekaluni.Kuwa na hali kama hii ingemzuia mtu kufanya kazi,kuabudu Mungu hekaluni na kuwa karibu na watu.

Mwaka wa 2020 ndio mwaka ambao ulimwengu mzima ulihisi athari ya Korona na bado tunaona athari zake katika mwaka wa 2021.Nchi nyingi zimefungwa;kuna uwoga wa kuambukizwa.Hivi ndivyo ilikuwa kwa huyu mtu wa ukoma.Pengine kwa miaka mingi,hangeweza kuchangamana na watu. Haya yalikuwa maisha gani ya upweke?

Yesu anataka kumponya mtu huyu.Anasema anataka kumponya,na neno hili ethelo kwa kamusi ya Strong G2309 linamaanisha kutaka sana,siyo kwamba ningependa nifanye.Na Zaidi ya hayo,Yesu akamfikia na kumguza.Tendo hilo lilinena kwa sauti kuliko maneno.Huyu mtu pengine hakuwa ameguzwa kwa muda mrefu,na hapa twaona huyu mwalimu mkuu akimguza.Tendo hilo lingefanya Yesu kuwa najisi kwa muda wa siku saba;yaani kwa kumguza mtu wa ukoma! Lakini alimguza na yule mtu akawa safi. Hakuwa tu mgonjwa tu lakini pia alikuwa najisi ,chafu

na mlaaniwa.Hakuponywa tu lakini pia alisafishwa.

Yesu anamwambia aende ajionyeshe kwa kuhani.Yesu anaonyesha kwamba Sheria ya Musa aliyopewa na Mungu,yaani Torati ,ni njema na yenye haki na bado ilikuwa ya kuitii.

Angechukua sadaka yake ya ndege wawili kwa kuhani ambaye atatumia damu kutoka kwa dhabihu ya ndege mmoja na kunyunyiza juu ya mwingine,ambaye ataachwa huru.Damu hiyo iliyomwagika ni ishara kwamba mtu huyo ametakaswa dhidi ya ugonjwa huo (Walawi 14:1-10)

Miaka michache baadaye,damu ya Yesu ilimwagiwa kwa kutakasa dhambi za mtu huyu na kutakasa dhambi za watu wote.

basi si zaidi damu yake Kristo,ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyoyana mawaa,itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu,mpate kumwabudu Mungu aliye hai? (Waebrania 9:14)

Wewe pia waweza kumwita Mungu aliye hai kupitia kwa Mwanawe ,Mwokozi Yesu kukutakasa kutoka kwa dhambi na kupata kuingia katika familia yake.

Maswali kutoka kwa Maandiko na Majibu Mafupi



Q. Kanisa lina msimamo gani kwa mpango wa ndoa na kuoa kwa mtu wa mbari tofauti anayetoka mbali?

A. Ndoa ni uamuzi mkubwa wa kudumu ambao mtu hafai kuingia kwa wepesi.Tofauti ya rangi na utamaduni zinaleta matatizo kwa ndoa.

Biblia inaonyesha kwamba Mungu aligawa watu wa rangi tofauti baada ya gharika.Japo,watu tofauti walichanganyikana (Kama vile Wapolinesi na Meksikana,ambao ni mifano miwili) na wengine wengi walifanya uamuzi kuhusu jambo hili na kuvuka ndoa ya kabila (kama Yusufu;tazama Mwanzo 41:45) na rangi (kama Musa;tazama Hesabu 12:1) .

Watu wenye tamaduni tofauti wanakuwa na ugumu katika ndoa. Vile wanaume na wanawake wanashirikiana katika ndoa inaweza kuwa tofauti sana kwa sababu ya utamaduni /au jadi.

Kwa mfano,miaka iliyopita ilipokuwa “si sahihi kisiasa” kufanya hivyo,maafisa wa serikali ya Marekani wangependekeza wanawake wa Marekani wasioe wanaume wa Uyunani.Hasa,onyo lilikuwa ni kwamba wakati wanaume Wayunani walikuwa wenye haiba wakati wanafanya uchumba na walikuwa watanashati,lakini vile wanawatendea wanawake baada ya kuwaoa na wanachotarajia kutoka kwao ni tofauti sana kuliko wakiolewa Marekani,na wanawake wa Marekani walikuwa wakijuta sana baada ya kuwaoa.

Wakati mfano huu haujatolewa kama onyo dhidi ya wanaume wa Uyunani,limetolewa kuwaonya watu kwamba kuna masuala makubwa na tamaduni tofauti na ni vizuri kujaribu kuyaelewa masuala hayo kabla hujafanya kosa kubwa.

Zaidi ya hayo,tamaduni nyingine zinawatendea wakwe na wengine tofauti.Hii ni pamoja na jinsi watakuwa karibu au jinsi watakuwa mbali na wanandoa.Wakati mwingine jambo hili laweza kuwa zuri lakini wakati mwingine linasumbua na kutatiza.

Tofauti ya kiuchumi pia inaweza kuwa sababu.Hata katika utamaduni wa kawaida,familia nyingine ina mali kuliko wengine-kwa hivyo kuna mazoea tofauti ya kutumia pesa.

Hata miongoni mwa wale wanaotoka kwa hali ya uchumi unayofanana ,jinsi pesa inatumika inatofautiana kutoka kwa familia moja hadi familia nyingine na pia kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Wakati unapofanya uchumba, jaribu kuwa mwangalifu kwa mtazamo wako wa pesa. Yeye anaweza kutumia pesa vizuri ama anaweza kutumia pesa vibaya kiasi cha kwamba mtakuwa na shida za pesa.

Kumbuka yafuatayo:

6 Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa. 7 Kwa maana hatukuja na kitu duniani, tena hatuwezi kutoka na kitu; 8 ila tukiwa na chakula na nguo tutaridhika na vitu hivyo. 9 Lakini hao watakao kuwa na mali huanguka katika majaribu na tanzu, na tamaa nyingi zisizo za maana, zenye kudhuru, ziwatosazo wanadamu katika upotevu na uharibifu. 10 Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha; ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na imani, na kujichoma kwa maumivu mengi. (1 Timotheo 6:6-10)

Mara nyingi mtu mmoja ataridhika, wakati mwingine hataridhika. Hiyo haimanishi kwamba wana ndoa wanapaswa kuwa wavivu na kukosa kujaribu kupata mengi iwezekanavyo, lakini kukosa kuridhika kunaweza kuleta usumbufu na mabishano. Sio kukosa pesa ndiko kunasababisha talaka katika tamaduni za Magharibi, lakini ni kukosa kulingana katika uwanja wa kifedha. Hiki ni kitu cha kuangaliwa wakati wa kufanya uchumba. Sababu za pesa ndizo zinasababisha talaka katika mataifa ya Magharibi.

Licha ya madai ya wengine, Biblia haina amri hasa dhidi ya Wakristo kuoa watu wa rangi ama kabila nyingine. Hata hivyo, kwa sababu ya shida za dunia (Hesabu

12:1-2) na pia ugumu katika ndoa, tunapendekeza kwamba watu wajaribu kuoa mtu ambaye wanaweza kulingana naye, na kuangalia pia vile watoto wao wa usoni wataathirika (jambo hilo linatofautiana kwa kila nchi /utamaduni).


Kulingana na Sensa wa mwaka wa 2010 kule Marekani, kiwango cha talaka ya watu wenye rangi tofauti kiko juu sana kuliko ya wana ndoa weupe. Mwinjilisti wa Kenya wa Kanisa la Mungu Linaloendelea Bwana Evans Ochieng aliripoti kwamba wakati Mwafrika ameoa mtu wa Magharibi, ndoa hiyo inasababisha shida nyingi. Kwa hivyo ndoa ya watu wenye tamaduni na rangi tofauti lazima iangaliwe.

Wakati sisi katika Kanisa la Mungu Linaloendelea haturuhusu ndoa ya watu wa mbari tofauti (kuoa nje ya rangi na tamaduni), hatuna mamlaka ya kibiblia ambayo tunatumia kupiga marafuku ,kwa hivyo hatupigi marafuku ndoa ya namna hiyo.


Basi, kuna shida kubwa katika ndoa ya rangi tofauti-ambayo Wakristo walio kwenye ndoa LAZIMA wazingatie. Katika sehemu nyingi ya ulimwengu, watoto watokao kwa ndoa kama hiyo wanatendewa vibaya. Hata wakiwa watu wazima,

Wakristo wanapaswa kuwapenda majirani kama vile wanavyojipenda wenyewe (Mathayo 22:39). Kwa hivyo wanapaswa kuweka MAANANI kwa jinsi ye yote wameoa anaweza kuleta athari ya kimwili ,kiroho na kihisia kwa watoto wake


Zaidi kuhusu uchumba na ndoa inapatikana katika kijitabu chetu cha mtandao, kinachopatikana kwa tovuti ya ccog.org, ambacho kinaitwa Dating: A Key to Success in Marriage, a practical dating guide for Christians




The Gospel of the Kingdom of God




Is God Calling You?



Is God's Existence Logical?



Prayer: What Does the Bible Teach?



Kuitekeleza Mathayo 24:14

Pamoja na Mathayo 28:19-20



Kanisa la Mungu *Linaloendelea* www.ccog.org

Taarifa za *Unabii wa Biblia za kilasiku* www.cogwriter.com

BIBLENEWSPROPHECY.NET Ujumbe wa redio wa kibiblia na mvuto wa kinabii.

CCOG.ASIA Tovuti inayolenga Asia. Ina Makala katika lugha ya Mandarini na Kichina na hata

Lugha ya Kiingereza, pamoja na nakala nyingi katika lugha nyingine ya Kiasia

CCOG.EU Tovuti hii inalenga Ulaya. Ina Makala mengi katika lugha ya Ulaya.

CCOG.IN Hii ni tovuti ilengayo India na ina Makala katika lugha nyingi za Kihindi.

CCOG.NZ Hii ni tovuti inayolenga wale wa Nyuzilandi.

CCOGAFRICA.ORG Hii ni tovuti ilengayo wale wa asili ya Afrika.

CCOGCANADA.CA Hii ni tovuti inayolenga wale walioko Kanada.

CDLIDD.ES La Continuación de la Iglesia de Dios. Hii ni tovuti ya Kihispania.

CG7.ORG Hii ni tovuti inayolenga wale wanaopenda Sabato ya Siku ya saba.

PNIND.PH Patuloy na Iglesya ng Diyos. Hii ni tovuti ya Ufilipino inayo Makala katika lugha ya Kiingereza na Tagalogi.



BibleNewsProphecy chaneli

CCOG Animations chaneli

CCOGsermones Spanish chaneli

ContinuingCOG sermon chaneli

ContinuingCOG Africa chaneli



BibleNewsProphecy channel



Kanisa la Mungu *Linaloendelea* (CCOG) pia hutumia majarida na magazeti ya kielektroniki, vitabu na barua za kila wiki kwa waumini wake katika kutekeleza Mathayo 24:14 pamoja na Mathayo 28:19-20.

Swahili Edition



COGAfrica chaneli

COGAnimations chaneli

COGTube sermon chaneli

Prophecy chaneli



BibleNewsProphecy chaneli

